# Mwongozo kwa Waalimu

## Wakati na Biblia Daraja la tatu na la nne

Mfululizo wa B
Masomo ya saba hadi ya kumi na mbili

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)
Imesajiliwa kama shirika la Hisani Uingereza (Namba 1186004)

**Dhamira**
Kuandaa masomo ya Biblia kwa ajili ya wadau ili kutumika kuwakilisha kweli ya Yesu Kristo kwa kizazi kijacho ulimwenguni kote.

**Maono**
Kufikia kizazi kijacho kwa lugha zao kwa kutumia mtaala wetu kamili kwa kukuza na kusaidia mtandao wa kimataifa wa wabia wanaojitolea.

## HABARI KWA UJUMLA

**Bible Educational Services hufanya nini:**

Bible Educational Services (BES) huchapisha masomo ya Biblia ya "Wakati na Biblia/Bibletime", "Maisha Mapya/New Life" na "Wakusanyaji/Gleaners" kwa Lugha ya Kiingereza na kusaidia vituo vya Shule ya Biblia kwa njia ya Posta pamoja na mashirika mengine ya namna hiyo yanayotumia masomo ya BES huko Uingereza na nchi zingine. BES hufanya hivi kwa kutembelea, kutoa ushauri, kutoa mafunzo na kuunganisha mashirika haya na mengine. Sasa hivi, BES inafanya kazi na vikundi mbalimbali kutoka nchi zingine, vinavyohusika na kutafsiri, kubuni, kuchapisha na kusambaza masomo. Masomo haya yanatolewa bure kabisa kwa kila mtoto.

Kwa mara ya kwanza, masomo ya Wakati na Biblia yalitumika huko Kusini mwa Ireland (Uingereza) miaka sitini iliyopita. Bible Educational Services (BES) wamechukua jukumu la uhariri wa masomo ya Wakati na Biblia kwa lugha ya Kiingereza na Lugha zingine. Kwa muda mrefu, Masomo ya Wakati na Biblia (Bibletime) yalichapishwa kwenye muundo wa A4 ambao uliwawezesha wanafunzi kutoka baadhi ya maeneo kutuma masomo yao kwenye kituo cha BES kwa ajili ya kusahihishwa kila baada ya wiki nne. Hivi karibuni, masomo ya miezi sita yamechapishwa kwa muundo wa A5. Muundo huu umefanya utumiaji wa masomo haya uwe rahisi na wakufaa zaidi kwa makanisa na shule ambazo hazina ufanisi mzuri wa mfumo wa njia ya posta. Tunawashukuru Every Home Crusade au Revival Movement huko Belfast Uingereza kwa kutuwezesha kufanya hivi.

Masomo ya BES ni ya kipekee kwa sababu yameandaliwa na vikundi mbalimbali kutoka makanisa na shule mbalimbali ambavyo vimezingatia mtaala (Syllabus). Masomo yamepangiliwa vizuri na yanamruhusu mwanafunzi kuyatumia kwa muda mrefu hadi atakapotimiza umri wa miaka ishirini. Masomo yanapatikana katika madaraja matano ambayo yamezingatia umri tofauti. Nayo ni, masomo kwa ajili ya watoto wa chekechea (chini ya miaka mitano), miaka mitano hadi saba, miaka nane hadi kumi, miaka kumi na moja hadi kumi na mitatu na miaka kumi na minne hadi kumi na sita. Kuna Mtaala wa miaka mitatu katika kila kikundi cha umri (angalia ukurasa wa 6). Vikundi hivi vya umri vinaweza kutofautiana kulingana na uwezo tofauti wa watoto. Rasilimali na masomo ya Wakati na Biblia yanawapa watoto fursa ya kujifunza Neno la Mungu, kujifunza Habari za Biblia na kujifunza kukabiliana na changamoto zinazotokea maishani mwao kulingana na mwongonzo wa Injili ya Bwana Yesu Kristo.

Nakala zilizochapishwa za masomo kwa Lugha ya Kiingereza zinapatikana kwenye tovuti ya BES /BES website – www.besweb.com au kwa katibu ofisi ya BES Uingereza. Yanapatikana pia kwa lugha zingine kwenye tovuti. Kwenye tovuti kuna nyaraka muhimu kwa mtu yeyote au shirika linalopenda kushirikiana nasi.

## Anuani za mawasiliano za BES

**Ofisi ya Uingereza (Northern Ireland) (Mhifadhi wa masomo yote ya Kiingereza)**
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Simu: +44 286 632 2462

**Katibu wa Uingereza**
Bw. Stephen Gillham,
Barua pepe: stephen.gillham@besweb.com

Tovuti: www.besweb.com
Barua pepe: info@besweb.com

**Mshirika Tanzania (Tanzania Partner)**
World Vision Tanzania
S.L.P. 6070 Arusha, Tanzania
Barua Pepe ya Mawasiliano: david_ombeni@wvi.org
Simu: +255 687 231 757

## MWONGOZO kwa WAALIMU

Mwanzoni, masomo ya Wakati na Biblia yaliandaliwa ili yatumike kwa njia ya posta kukiwepo na kituo cha Shule ya Biblia kwa njia ya posta. Sasa hivi, masomo yanaendelea kutumika kwa wingi hata kwenye sehemu ambazo hazina ufanisi wa kutumia mfumo wa posta au hakuna kabisa mfumo wa posta hasa katika makanisa na shule zilizopo Afrika, India na maeneo mengine. Mwongozo wa kufundisha umeandaliwa kwa wale wanaotumia masomo ya Wakati na Biblia katika hali kama hizo. Mwongozo wa kufundisha katika kitabu hiki umeandaliwa kutumika kwa masomo ya daraja la tatu na la nne kwa watoto wenye umri wa wastani wa miaka 11-16 na zaidi.

Kila Mwongozo wa kufundisha hufuata vifungu vile vile vya Biblia vilivyopo katika somo la Wakati na Biblia. Masomo ya Wakati na Biblia na Mwongozo vimeandaliwa vitumike kwa kila wiki. Masomo ya mwezi Aprili yanahusu Pasaka na masomo ya mwezi Desemba yanahusu Krismasi.

Baadhi ya sehemu watakuwa wanatumia masomo yaliyo katika toleo la A4 la kila wiki na wengine watakuwa wanatumia kitabu cha A5 chenye masomo 24 ndani yake. Kwa kawaida, mwalimu au kiongozi hutoa somo la mwezi toleo la A4 na kila wiki sehemu ya kazi hujazwa kanisani au shuleni au hupelekwa nyumbani na kurejeshwa wiki inayofuatia. Mwishoni mwa mwezi, mwalimu au kiongozi hukusanya somo na kwenda kusahihisha kama inavyotakiwa na kumrudishia mwanafunzi/mtoto kazi iliyosahihishwa mapema iwezekanavyo.

Unapotumia kitabu, mwisho wa kila kipindi, vitabu hukusanywa na kusahihishwa. Tumegundua katika sehemu nyingi kuwa, hili haliwezekani. Hivyo basi, pale darasani masomo yanaweza kugawanywa kwa wanafunzi wengine na mwalimu au kiongozi ataongoza usahihishaji wa somo na wanafunzi watasahihisha masomo ya rafiki zao na kutoa maksi. Nyuma ya kitabu kuna sehemu kwa ajili ya kuweka maksi ya kila somo la mwezi na pia mahali pa maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Pia kuna cheti ambacho mwanafunzi anaweza kupewa kinachoonesha asilimia ya alama ambazo mwanafunzi amepata kwa masomo ya miezi sita.

Tutashukuru kama tutapata mrejesho kuhusu matumizi ya Miongozo ya Waalimu na kwa ajili ya vitabu vya Wakati na Biblia na mrejesho huo utumwe kwa stephen.gillham@besweb.com.

## MAANDALIZI KWA WAALIMU

Hatupendi kutoa shinikizo na kutokuwapa waalimu fursa ya kufanya mambo kwa njia zao wenyewe kulingana na mawazo na mipango yao wenyewe. Haya ni mapendekezo yanayoweza kutumika kwenye utumiaji wa masomo ya Wakati na Biblia.

- **Elewa habari vizuri –** Waalimu wanapaswa kuelewa habari ya Biblia vizuri kwa kadri iwezekanavyo na vile vile somo la Wakati na Biblia linaloendana na habari hiyo ya Biblia. Ni jambo zuri kwa mwalimu kukamilisha somo la Wakati na Biblia kabla ya kipindi. Mwongozo wa kila somo unapaswa kutumiwa kwa umakini kama chombo cha kumsaidia mwalimu anapojiandaa kwa ajili ya somo.
- **Elewa funzo ambalo watoto wanastahili kupata au kujifunza –** Juu ya kila mpangilio wa somo utaona maneno ‘Tunajifunza kuwa’ ikifuatiwa na makusudio mawili ya kujifunza ambayo tunatumaini kwamba watoto watayaelewa baada ya kumsikiliza mwalimu akifundisha na kukamilisha somo la Wakati na Biblia. Kusudio la kwanza la kujifunza linahusu ufahamu wa habari na la pili linamtia moyo mtoto kufikiri juu ya ufahamu huo, kuutumia na kuuitikia. Makusudio haya ya kujifunza ni sentensi kamilifu na fupi ya mawazo au kweli kuu zinazofundishwa katika somo. Waalimu wanaweza kuzitumia kwa ajili ya tathimini zao binafsi za ufundishaji na mafunzo ambayo watoto wamepata.
- **Toa Utangulizi –** Kwa masomo yote, tunaanzia mahali ambapo watoto wapo katika uzoefu wao wa hali husika. Tumependekeza njia kadhaa ambazo zinaweza kutumika kufanya utangulizi wa habari ili kuwawezesha watoto kuhusika katika kujadili mwanzo wa habari.
- **Fundisha –** Tumetoa dondoo muhimu katika habari. Tunaamini kwamba waalimu hawatazinukuu wakati wanafundisha habari lakini watakuwa na uelewa mzuri wa habari na wataweza kuifundisha katika njia inayofurahisha na kusisimua. Mwalimu atahitaji watoto waelewe mafunzo muhimu kutoka kwenye habari na kuwasaidia kuuelewa mwitikio watakaoupata kutoka kwenye habari waliyojifunza. Kwa usahihi, tumejaribu kuweka pamoja baadhi ya maelezo kwa ajili ya kufundisha habari. Haya yameandikwa katika maandishi *YA MCHALAZO (Italics)*.
- **Jifunze –** Kuna Mstari muhimu ambao umewekwa katika kila habari. Katika baadhi ya maeneo, kuna Mistari muhimu miwili. Mstari huu ulioongezwa unaweza kuwa rahisi kwa watoto kujifunza. Tunatumaini kwamba, watoto watajifunza Mistari muhimu na watakumbushiwa mstari huo mara nyingi iwezekanavyo ili waanze kujenga ufahamu wa Mistari muhimu ya Biblia.

- **Kamilisha –** Katika mazingira ya shule, utatambua uwezo wa watoto kwenye kukamilisha kazi na kiasi cha usaidizi ambao wanauhitaji kutoka kwa mwalimu. Kwa baadhi yao, itahitajika mwalimu asome maandishi katika somo na watoto kufuatilia habari ambayo sasa watakuwa wanaielewa. Watoto wengine wanaweza kusoma maandishi ya somo peke yao. Kwa hali yoyote kati ya zilizotajwa, ni wazo zuri kuwahamasisha watoto wawe makini na kuwapa maelekezo muhimu yanayohusiana na maswali. Kama unatumia masomo ya Wakati na Biblia katika maeneo ambayo siyo shule, ni muhimu uwepo ili watoto wasichukulie masomo kama kazi isiyo na mvuto au kama mtihani. Masomo haya yanapaswa kuwa ya kufurahisha na kutia moyo. Ni muhimu kuwasifia watoto wanapoendelea kufanya masomo na kujibu maswali.
- **Kumbuka –** Tunashauri matumizi ya maswali mafupi na maigizo ili kuwasaidia watoto kujifunza na kurudia habari ili kuielewa vyema.
- **Kuonesha –** Tunatambua kuwa katika baadhi ya mazingira, sio rahisi kupata vielelezo au video. Lakini, ni muhimu kadri iwezekanavyo kuwa na picha au vitu vinavyoweza kuwasaidia watoto kuielewa habari vizuri zaidi. Vielelezo vitakuwa muhimu sana wakati ambapo mwalimu anaelezea habari. Kadri iwezekanavyo kwenye kila somo, tumetoa maelezo kuhusu picha kutoka kwa picha za www.freebibleimages.org (FBI) ambazo zinaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti yao. Mwishoni mwa Mwongozo huu kuna viambatanisho vyenye viungo (hyperlinks) vya picha kadhaa kutoka kwenye tovuti ya Free Bible Images ambazo zinafaa kila habari ya Biblia.
  Kama kuna kinakilishi (photocopier), baadhi ya picha za Bibletime zinaweza kufanywa kuwa kubwa, kupakwa rangi na kutumiwa kufundisha.

## Kupangilia Muda

- **Ratiba –** Tumeweka ratiba sawa kwenye mwongozo wa kufundisha kila somo lakini mwalimu anaruhusiwa kubadilisha ratiba hii mara kwa mara kulingana na mahitaji ya darasa lake/ watoto anaowafundisha.
  1. Utangulizi na kuwaambia watoto habari husika – Takriban dakika 15
  2. Kufundisha Mstari muhimu – dakika 5 hadi 10
  3. Kujaza nakala ya somo – dakika 20
  4. Maswali na shughuli zinginezo- dakika 5 hadi 10

Kumbuka msemo muhimu:

“Niambie na nitasahau,
Nioneshe na nitakumbuka,
Nihusishe na nitaelewa”

## Mtaala wa Wakati na Biblia

| | Daraja 0 (Chekechea/ Kabla ya Kuanza Shule) Daraja la Kwanza (Miaka mitano hadi saba) Daraja la Pili (Miaka nane hadi kumi) | Daraja la Tatu (Miaka kumi na mmoja hadi kumi na mitatu) | Daraja la Nne (Miaka kumi na minne na zaidi) |
|---|---|---|---|
| SOMO LA KUANZIA | Somo la kuanzia – Utangulizi | Somo la kuanzia – Utangulizi | Somo la kuanzia – Utangulizi |
| MFULULIZO WA A | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Ibrahimu<br>6. Ibrahimu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa Kwanza<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo na Kuanguka<br>2. Matukio ya Kwanza-Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya Ukristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA B | 1. Maisha ya kwanza ya Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Mifano<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Walioandika vitabu vya Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Yusufu<br>8. Matendo ya Mitume 2: 42 – Njia iliyoko mbele<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Amri<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA C | 1. Danieli<br>2. Miujiza zaidi<br>3. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu na Samweli<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>3. Miujiza zaidi<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8 Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu ambao Mungu aliwatumia – Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Kristo<br>3. Nguvu za Bwana<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu zaidi wa Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi |

| | **B7 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Kwanza – Maisha ya Yusufu**<br>**Mada – Wapelelezi nchi ya Misri** | **B7 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Kwanza – Maisha ya Yusufu**<br>**Mada – Majaribu ya Ujana Wake** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 41: 46-57 na 42: 1-38***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Hesabu 32: 23***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Hatuwezi kutenda dhambi halafu tuepuke adhabu yake.<br>2. Lazima tuungame dhambi zetu kabla ya kupokea msamaha ambao ni Bwana Yesu tu anaweza kuutoa. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 39: 1-23 na 40: 1-23***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 39: 21***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yusufu hakukubali kushindwa na majaribu.<br>2. Bwana alikuwa pamoja na Yusufu katika utumwa, majaribu, na kifungo. Yusufu alimtumaini na kumtii Bwana. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waeleze wanafunzi kwamba Wamisri walitegemea mazao yao wenyewe kwa ajili ya chakula na miaka saba ya njaa ilikuwa ni kipindi kigumu sana kwa watu. Mahindi yalikuwa zao la thamani katika siku hizo kwani yalikuwa yakitumika sana kwa chakula na yaliweza kuhifadhiwa kwa muda mrefu. Yalitumiwa pia kwa ajili ya kupata pesa. Eleza kwamba Misri ilikuwa na hali nzuri zaidi kiuchumi wakati wa njaa kuliko nchi jirani kwa sababu ya Mto Nile. | Wakumbushe wanafunzi kuhusu habari hii tangu B6 hadi sasa. Wakati huu Yusufu yuko Misri, lakini shida zake hazijaisha. Mungu anaruhusu apitie hali ngumu, ili awe tayari kukabiliana na changamoto katika siku zijazo. Wakumbushe wanafunzi kwamba wakati mwingine Mungu hutupima kwa kuruhusu tupitie majaribu ambayo yanaweza kutufanya tuimarike kwa ajili ya kukabili changamoto za siku zijazo. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Njaa inadumu kwa miaka saba ***(mstari wa 54)*** na Yusufu ndiye pekee anayeweza kutimiza mahitaji ***(mstari wa 55)*** kutoka kwenye chakula kingi cha nafaka kwenye ghala za Farao.<br>2. Ilibidi ndugu zake Yusufu washuke kwenda Misri kutafuta mahindi kwa sababu ya njaa. ***(42: 1-3)***<br>3. Yusufu aliwatambua ndugu zake, lakini wao hawakumtambua. ***(42: 7)*** Akawatia gerezani kwa siku tatu.<br>4. Yusufu anawafanyia ndugu zake vitendo ambavyo anajua vitawafanya watambue jinsi walivyomkosea. ***(42:21)*** Baada ya hapo ndipo awasamehe.<br>5. Kumbukumbu zao na dhamiri zao zinawathibitishia kuhusu hatia yao, na wanaelewa sababu ya dhiki wanayoipata.<br>6. Licha ya dhambi yao, Yusufu anawalilia ***(mstari wa 24)*** na kuwapatia chakula kwa ajili ya safari yao ya kurudi kwa baba yao Yakobo, lakini anamtia Simoni gerezani na kuwaagiza kwamba Benyamini, mtoto wa mwisho ateremshwe Misri.<br>7. Yakobo anakasirika sana wanapomwambia yote yaliyotokea na anasema kamwe hataruhusu Benyamini ashuke kwenda Misri. ***(42: 38)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha somo la kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Wapelelezi nchi ya Misri. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yusufu alitumia vizuri hali yake kama mtumwa huko Misri na mara akapata kuaminiwa na Potifa. ***(39: 2)***<br>2. Mke wa Farao alimshtaki kwa uwongo Yusufu kwamba amemshambulia na hivyo kumfanya afungwe gerezani. ***(39: 11-20)*** Hata hivyo, Yusufu alikuwa kijana mwadilifu ambaye aliendelea kumtegemea na kumtumaini Mungu, bila kujali hali iliyojitokeza na Mungu akamfanikisha kwa kugeuza hali hii na kumfanya Yusufu kuwa msimamizi wa gereza. ***(39: 21-23)***<br>3. Wafungwa wawili katika gereza hilo walikuwa na ndoto na Yusufu aliweza kuzitafsiri. ***(40: 8)***<br>4. Tafsiri ya Yusufu ya ndoto ya mkuu wa wanyweshaji ilikuwa ujumbe wa uhai kwa kuwa aliachiliwa kutoka gerezani, lakini tafsiri ya ndoto ya mwokaji ilikuwa ujumbe wa kifo kwa kuwa mkuu wa waokaji aliuawa.<br>5. Yusufu alimwomba mnyweshaji kumkumbuka na kuomba msaada wa Farao wakati alipoachiliwa lakini alisahau yote kuhusu Yusufu. ***(40: 14 & 23)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Majaribu ya ujana wake. |
| **REJELEA SOMO** | Jadili na wanafunzi jinsi Mstari Muhimu unavyotoa muhtasari wa somo. | Jadili na wanafunzi jinsi Mstari Muhimu unavyotoa muhtasari wa somo kuhusu:<br>1. Maisha ya Yusufu katika nyumba ya Potifa; na<br>2. Maisha ya Yusufu gerezani. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kumbuka umuhimu wa kuigeuzia dhambi mgongo na kumgeukia Bwana Yesu kwa ajili ya msamaha wake.<br>2. Umuhimu wa kuelewa ***1 Yohana 1: 9: 'Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.'***<br>3. Kumbuka K, A, K ya Wokovu - K- Kubali umetenda dhambi. A- Amini kwamba Bwana Yesu alikufa kwa ajili yetu msalabani. K- Kiri kwamba Yesu ni Bwana wa maisha yako. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Tunatakiwa tusikubali kuanguka katika majaribu lakini tumwombe Bwana kila siku atusaidie kuyashinda.<br>2. Siri ya kuwa shahidi mzuri wa Bwana ni kutambua fursa ambapo tunaweza kumhusianisha Bwana Yesu na uzoefu wa mtu mwingine, katika juhudi za kumvuta amwamini Mwokozi<br>3. Angalia Masomo Zaidi Yanayopendekezwa, ***Waefeso 6: 13-17*** na ***Yakobo 1: 12-18,*** na fikiria jinsi tunavyoweza kushinda majaribu katika maisha yetu. |

| | B7 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Pili – Maisha ya Yusufu<br>Mada – Benyamini na habari mbaya! | B7 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Pili – Maisha ya Yusufu<br>Mada – Kuinuliwa kwake ikulu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 42: 35-38; 43: 11-14, 24-31, 44: 1-33***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Efeso 4: 32***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yuda, aliyeungana na kaka zake kumuuza Yusufu utumwani, sasa anajitolea kuwa mtumwa yeye mwenyewe ili kumwokoa Benyamini ***(44: 33)***<br>2. Mungu anaweza kugeuza watu wenye mioyo migumu na kusababisha mabadiliko kamili katika maisha yao. | **Neno la Biblia:** ***Genesis 41: 1-45***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 41: 38***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yusufu aliinuliwa haraka akawa mtu mkuu - kutoka hali ya kuwa mtumwa hadi kuwa Waziri Mkuu wa Misri. Katika hali zozote tunazopitia, tunapaswa kuziona kama sehemu ya mpango wa mafunzo ambao Mungu amekusudia kwa ajili ya maisha yetu.<br>2. Kama vile Farao alivyotambua kwamba Yusufu alikuwa 'mtu mwenye Roho wa Mungu ndani yake' ***(41: 38)***, vivyo hivyo wale wanaokujua wanapaswa kumuona Mungu ndani yako, kwa matendo yako ya huruma na maisha yako ya utauwa |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadili na wanafunzi jinsi ambavyo dhambi ya kaka zake Yusufu haikuleta tu dhiki kwao wenyewe lakini pia ilileta maumivu makubwa ya moyo kwa baba yao Yakobo. Eleza jinsi dhambi inavyoweza kuwa na athari kubwa kwa familia zetu na marafiki zetu, pamoja na kwetu sisi wenyewe. | Yusufu aliitwa kutoka gerezani akasimame mbele ya Farao. Uwezo wa Yusufu aliopewa na Mungu kumweleza Farao mambo yote kuhusu ndoto yake ulimvutia sana Farao kiasi kwamba alimpa Yusufu ofisi ya juu ya 'Waziri Mkuu'. ***(Mwanzo 41: 41)*** Yusufu alikuwa mwaminifu kwa Mungu kupitia hali ngumu (Funzo la Kwanza) na Mungu alikuwa mwaminifu kwake. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Njaa inaendelea na ndugu wanarudi tena Misri kupata chakula. Yakobo anasita sana kumruhusu Benyamini aende Misri. ***(43: 11-13)*** Yusufu tu ndiye angeweza kutosheleza hitaji lao na kukabiliana na shida zao.<br>2. Ndugu wote wanaalikwa nyumbani kwa Yusufu kwa chakula, na bado hawamtambui. ***(43: 16)***<br>3. Ndugu wenye hofu wanafurahia karamu iliyoandaliwa na Yusufu katika kasri lake. Yusufu analia anapomwona mdogo wake Benyamini. ***(43:30)***<br>4. Anaamuru kikombe chake cha fedha kuwekwa kwenye gunia la Benyamini na anadai kwamba Benyamini amekiiba na lazima aadhibiwe. ***(44: 17)***<br>5. Wakati huu wote, Yusufu anajaribu na kutathmini kama kaka zake wako tayari kwa msamaha, ambao yuko karibu kuwapa.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Benyamini na habari mbaya! | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Wachawi na watu wenye hekima hawakuweza kutafsiri ndoto za Farao, lakini Mungu alikuwa amefunua maana yake kwa Yusufu. ***(41: 8)***<br>2. Ujuzi wa Yusufu kuhusu Mungu ulimsaidia kutafsiri ndoto na tena anampa sifa Mungu. ***(41: 16)***<br>3. Yusufu alimpa Farao mpango wa kuishi katika miaka saba ya njaa ambao uliokoa maisha ya watu wengi huko Misri na wale wa familia yake mwenyewe walioishi mbali sana. ***(41: 33-36)***<br>4. Yusufu anainuliwa na kufanywa mtawala juu ya nchi ya Misri. Alipewa jina jipya na akapewa binti wa afisa mashuhuri wa Misri kuwa mkewe, kuonyesha jinsi alivyoheshimiwa sana. **(41: 41-45)**<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kuinuliwa kwake ikulu. |
| **REJELEA SOMO** | Waeleze wanafunzi kuwa:<br>1. Kuna utupu maishani mwetu mpaka tukiri dhambi zetu na kuja kwa 'Yusufu wa kiroho', ambaye ni Bwana Yesu, kwa ajili ya msamaha.<br>2. Sikukuu ya baraka inawangojea wale waliosamehewa, hasa katika maisha yajayo Mbinguni. | Waulize wanafunzi maswali kuhusu (i) ndoto, (ii) tafsiri zake, na (iii) kuinuliwa kwa Yusufu ili kuwasaidia kujibu maswali kwa usahihi katika Funzo la Pili. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Zingatia kuwa dhambi husababisha dhiki.<br>2. Tunapotubu na kuungama dhambi zetu Bwana Yesu anakuwa tayari kutusamehe.<br>3. Bwana Yesu anapotusamehe tunapaswa na sisi kuwasamehe wale wanaotukosea. ***(Waefeso 4: 32)*** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kama vile Yusufu alivyokuwa tayari kwa lolote kwa sababu ya uhusiano wake sahihi na Mungu, ndivyo tunavyopaswa kujifunza kutokana na mfano wake. Ikiwa sisi ni Wakristo, sala na Kujifunza Biblia ni muhimu ili kujua mapenzi ya Mungu na mwelekeo wa maisha yetu.<br>2. Soma Masomo Zaidi Yanayopendekezwa na ugundue mwandishi wa Zaburi Daudi na Mtume Paulo walisema mambo gani juu ya Yusufu miaka mingi baada ya kifo chake na utumie masomo haya kwa ajili ya maisha yako mwenyewe. ***Zaburi 105: 16-22*** na ***Matendo 7: 9-10***<br>3. Wakati wote Yusufu alikuwa mwangalifu kumpa Mungu sifa na sisi tunapaswa kuwa waangalifu kufanya vivyo hivyo. Kuchukua heshima kwa ajili yetu wenyewe ni kuiba heshima ya Mungu. |

| | **B7 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Tatu – Maisha ya Yusufu**<br>**Mada – Msamaha na habari njema!** | **B7 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Tatu – Maisha ya Yusufu**<br>**Mada – Tabia yake ya kujali** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 44: 18-34; 45: 1-14, 25-28***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 45: 9***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ijapokuwa kaka zake Yusufu walitaka kumwondoa duniani, Mungu alitumia matendo yao mabaya kuhifadhi maisha yao, kuokoa Misri na kuandaa njia kwa ajili ya mwanzo wa taifa la Israeli<br>2. Kama vile Yusufu alivyokataliwa na baadaye akawasamehe ndugu zake, Mungu hutusamehe na kutubariki ingawa sisi tumemkataa. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 42 na 43***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Warumi 14: 11-12***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ndugu zake Yusufu lazima waletwe kuona na kukiri dhambi zao kabla ya kusamehewa.<br>2. Kama vile kaka zake Yusufu walivyoinama chini kujitiisha kwake, vivyo hivyo kila mmoja wetu atainama mbele ya Bwana Yesu Kristo katika siku inayokuja na kumtambua kama Bwana. |
| **TOA UTANGULIZI** | Yusufu alipoona kwamba ndugu zake wamejutia kweli, alidhihirisha kuwa yeye alikuwa ni nani kwao na akasema: ***"Mimi ni Yusufu." (Mwanzo 45: 4)*** Jadili na wanafunzi jinsi 'Yusufu wa mbinguni, Bwana wetu Yesu Kristo', pia alivyojitaja mwenyewe kama 'mimi ni' katika maneno yafuatayo: ***Yohana 6: 35 - mkate wa uzima; Yohana 8: 12 - nuru ya ulimwengu; Yohana 10: 7 - mlango; Yohana 10: 11 - mchungaji mwema; Yohana 11:25 - ufufuo na uzima; Yohana 14: 6 - njia; Yohana 15: 1 - mzabibu.*** | Mara ya mwisho Yusufu alipowaona ndugu zake, karibu miaka ishirini iliyopita, walimuuza kwa wafanyabiashara wa watumwa wa Midiani kwa vipande ishirini vya fedha. Lazima Yusufu alikuwa akijiuliza kama bado walikuwa waovu na wenye hila au walikuwa wamebadilika baada ya miaka kupita. Aliamua kuwapitisha kwenye majaribio machache ili kugundua zaidi tabia yao! |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Kikombe cha fedha kilikuwa ishara ya mamlaka ya Yusufu na kukiiba ni kosa kubwa. Sasa ndugu zake walikuwa na wasiwasi kwamba Benyamini anaweza kudhuriwa hivyo wakati wa kurudi kwenye ikulu ya Yusufu, Yuda anajitolea kupewa adhabu ya Benyamini. ***(44: 33)***<br>2. Badala ya kupewa adhabu ndugu walipokea msamaha ***(45: 5)*** na Yusufu anawaelezea jinsi Mungu alivyokuwa akiandaa makusudi Yake katika maisha yake mwenyewe, licha ya yale waliyokuwa wamefanya.<br>3. Ndugu zake wanarudi kwa Yakobo na habari njema kwamba Yusufu yu hai na kumwonyesha zawadi zinazotoka kwa Yusufu. ***(45: 26-27)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Msamaha na habari njema! | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Ndugu zake Yusufu wanakuja Misri kwa ajili ya hitaji lao la kununua nafaka. Yusufu anazungumza nao 'kwa ukali' jambo linaloonesha kwamba atasababisha watambue dhambi zao kabla ya kusamehewa. ***(42: 6-7)***<br>2. Yusufu aliwatia gerezani kwa siku tatu. Katika dhamiri zao wakajua wamemkosea Yusufu na kwa hivyo wakakiri hatia yao. ***(42: 21)***<br>3. Ingawa Yusufu anawaadabisha ndugu zake, anafanya hivyo kwa upendo kwani tunaambiwa katika Mwanzo 42: 24 kwamba alilia. Hapa tunaona neema ya kweli kwa vitendo wakati Yusufu anaendelea kuonyesha upendo kwa kaka zake ambao hawakustahili.<br>4. Katika safari yao ya pili kwa Yusufu, wakiwa na Benyamini pamoja nao, ndugu wanainama kwa heshima mbele yake na kutambua mamlaka yake. ***(43: 26-28)*** Hapa tunaona ndoto ya Yusufu, katika ***Mwanzo 37: 7*** ikitimia. Hii inatuonyesha Neno la Mungu lina pumzi ya Mungu na ni kweli!<br>5. Yusufu anaguswa sana moyoni wakati mwishowe anapomwona ndugu yake Benyamini na anaingia kwenye chumba kingine na kulia. ***(43:30)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Tabia yake ya kujali. |
| **REJELEA SOMO** | Unganisha somo hili na Mstari Muhimu:<br>***"Mungu amenifanya bwana wa Misri yote!"*** na ***"Unishukie usikawie."*** Jadili na wanafunzi majibu ya Yakobo ya kufurahishwa na misemo hii miwili. ***(45: 9)*** | Jifunze Mistari Muhimu miwili na jadili na wanafunzi jinsi inavyotoa muhtasari wa somo hili. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Umuhimu wa kujua Bwana Yesu yuko hai Mbinguni, na ni Bwana wa wote, kama vile Yusufu alivyokuwa hai Misri na mtawala juu ya yote.<br>2. Umuhimu wa kuelewa kwamba Bwana Yesu hatupi msamaha peke yake bali pia anatupa baraka tele tunapomtumaini.<br>3. Kwa mara nyingine, wakumbushe wanafunzi juu ya hitaji la sisi kufuata mfano wa Mungu wa msamaha kwa kuwasamehe wengine, kama Bwana Yesu alivyofundisha katika maombi Yake kwa wanafunzi. ***(Mathayo 6: 12)*** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Tunajifunza nini juu ya neema ambayo Bwana Yesu anatoa katika ***Warumi 5: 21***?<br>2. Kama vile Yusufu alivyoonesha upendo kwa ndugu zake ambao walimkosea, tunaona upendo mkubwa zaidi uliooneshwa na Bwana Yesu alipokufa kwa ajili ya wenye dhambi kama sisi pale Kalvari. Soma ***Luka 23: 34*** na uutafakari.<br>3. Ndoto ya Yusufu katika ***Mwanzo 37: 7-8*** ikawa ukweli katika ***Mwanzo 43: 26.*** Soma Masomo Yanayopendekezwa Zaidi, ***Zaburi 51*** na ***Wafilipi 2: 9-11*** na fikiria jinsi masomo haya pia yanavyosisitiza hitaji la kukiri dhambi zetu na haja ya kutambua kwamba 'Yesu Kristo ni Bwana.' |

| | B7 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Maisha ya Yusufu<br>Mada – Pamoja huko Misri | B7 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Maisha ya Yusufu<br>Mada – Msamaha wake kamili |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 46: 1-7; 26-34***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 50: 20***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Uaminifu wa Yusufu uligusa familia yake yote na kuwaletea baraka nyingi.<br>2. Yusufu ni mfano halisi wa ahadi ya Bwana katika ***1 Samweli 2:30*** ambayo inasema: ***"wanaoniheshimu nitawaheshimu."*** | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 44 na 45***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Warumi 5: 10***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ndugu zake Yusufu walipokiri dhambi zao urafiki wao na Yusufu ulirejeshwa na sisi tunapokiri na kutubu dhambi zetu, tunaweza kuwa na urafiki wa kweli na wenye maana na Bwana Yesu.<br>2. Kama vile Yusufu alivyowapatia baraka nyingi ndugu zake huko Misri vile vile Bwana Yesu anawapatia baraka nyingi wale walio wake na atawapeleka Mbinguni kutakapokuwa na furaha ya milele. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waeleze wanafunzi jinsi Mungu anavyotimiza mpango wake katika maisha ya Yusufu. Familia yake yote ilitoka Kanaani ili kuishi naye huko Gosheni, Misri. Hata hivyo, Kanaani iliahidiwa kwa Ibrahimu na uzao wake, lakini wakati huu Mungu alikuwa akiitoa familia ya Yusufu mbali na ushawishi mbaya wa Wakanaani ambao walikuwa wamempa Mungu kisogo. Hata hivyo, kama vile Mungu alivyokuwa ameahidi, taifa la Israeli lilirudi Kanaani. | Katika somo lililopita tulijifunza jinsi Yusufu alivyotenda kwa ustadi kuwasaidia ndugu zake kukiri dhambi zao. Njia sasa iko wazi kwa Yusufu kuwasamehe na ndugu zake kupatanishwa kabisa na urafiki wao uliovunjika kurejeshwa. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu anamwambia Yakobo aondoke nyumbani kwake na kusafiri kwenda nchi ngeni ya mbali na kumhakikishia kwamba atamtunza. ***(46: 2-3)***<br>2. Familia nzima pamoja na mali zao zote inaenda Misri. ***(46: 5-7)***<br>3. Familia ya Yakobo inawasili Gosheni na mkutano wa machozi unafanyika kati ya Yusufu na Yakobo. ***(46: 29)***<br>4. Baada ya kifo cha Yakobo, ndugu waliogopa kwamba Yusufu atalipiza kisasi lakini kwa mshangao sio tu kwamba aliwasamehe bali alijitolea kuwatunza wao na familia zao. ***(50: 15-21)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Pamoja huko Misri. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Kabla ya ndugu zake kuondoka ili kurudi kwa baba yao Yakobo, huko Kanaani, Yuda anajitolea kukaa Misri na kutumikia kama mtumwa badala ya Benyamini. Haya yalikuwa ni mabadiliko tangu wakati walipomuuza Yusufu kuwa mtumwa na kumsababishia Yakobo miaka mingi ya maumivu ya moyo! Neema ya Mungu sasa ilikuwa ikifanya kazi moyoni mwake. ***(44: 33)***<br>2. Yusufu anajiweka wazi kwa ndugu zake na kuwaambia Mungu amegeuza mabaya kuwa mema. ***(45: 4-5)***<br>3. Yusufu analia, anamkumbatia Benyamini, na kuwabusu ndugu zake wote. ***(45: 14)***<br>4. Farao aliwaambia ndugu za Yusufu wamlete baba yao na familia zao Misri naye atawapa mahitaji yao. ***(45: 17-19)***<br>5. Ndugu wanamwambia Yakobo kuwa Yusufu yuko hai na alipoona magari yaliyotumwa kuwaleta wote Misri, Yakobo alijua Yusufu yuko hai na atakutana naye tena! ***(45: 25-28)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Msamaha wake kamili. |
| **REJELEA SOMO** | Waulize wanafunzi kwa uangalifu ili maswali hayo yawasaidie katika kujaza majibu ya maswali katika somo hili la 4 | Vuta usikivu wa wanafunzi kuhusu jinsi 'Habari Njema' katika habari hii kuhusu Yusufu inavyofanana na 'Habari Njema' kuhusu Bwana Yesu<br>1. Vuta usikivu wa wanafunzi kuhusu jinsi 'Habari Njema' katika habari hii kuhusu Yusufu inavyofanana na 'Habari Njema' kuhusu Bwana Yesu Kama vile Yusufu alivyokuwa hai, Yesu yuko hai leo<br>2. Kama vile Yusufu alivyokuwa mtawala huko Misri vivyo hivyo Bwana Yesu ni Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana.<br>3. Kama vile Yusufu alivyotunza familia yake, Bwana Yesu ametupatia kila kitu tunachohitaji kwa ajili ya wokovu; na<br>4. Kama vile Yusufu alivyoleta familia yake Misri, Bwana Yesu anataka sisi tuje kwake ili tupate wokovu na atupeleke Mbinguni milele. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kama ambavyo lazima Yusufu alikuwa akijiuliza mara nyingi kuhusu maisha yake ya siku zijazo yatakavyokuwa; hatuwezi wakati wote kujua kitakachotokea. Lakini, kama Wakristo, tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu ataheshimu uaminifu wetu.<br>2. Mungu anaweza kugeuza makusudi mabaya na serikali ovu za ulimwengu huu wa leo ili kusababisha matokeo Yake aliyoyakusudia. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Tunahitaji kuwa tayari kukiri na kutubu dhambi zetu, na kumtumaini Bwana Yesu ambaye alikufa kwa ajili yetu. Ndipo tutajua msamaha na lazima tuwe tayari kuwasamehe wengine.<br>2. Mungu alikuwa pamoja na Yusufu na jambo hili lilisimuliwa na Stefano miaka kadhaa baadaye katika Agano Jipya kabla ya kuuawa kama shahidi kama ilivyo katika Maandiko Yanayopendekezwa. ***(Matendo 7: 12-15)*** |

| | B8 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Kwanza – Waandishi wa Injili<br>Mada – Mathayo | B8 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Kwanza – Njia iliyoko mbele<br>Mada – Wakristo kuwa pamoja |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 9: 9-13; na 27: 37-42***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 16: 16***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alipomwita Mathayo, Myahudi, mtoza ushuru, aliitika mara moja na kumfuata Yesu.<br>2. Wayahudi wengi, hata hivyo, walikataa kumpokea Yesu na, kwa sababu hiyo, alisulubiwa. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 2: 41-44, Matendo 4: 32-35***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 2: 42***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Watu walipokuwa Wakristo, walitambua umuhimu wa kushirikiana pamoja kama jamii, wakitafuta kukua katika imani yao.<br>2. Pia walitafuta kusaidiana kwa njia yoyote iliyowezekana na kuhudumiana kwa mali zao. |
| TOA UTANGULIZI | Waeleze wanafunzi kwamba Mathayo alikuwa afisa wa forodha. Watu hawa walichukiwa na Wayahudi kwa sababu ya upotovu wao, ushuru mkubwa waliokusanya kutoka kwa watu na kwa sababu walitimiza masilahi ya Dola ya Kirumi ambayo ilikuwa ikiwatawala Wayahudi wakati huo. | Waeleze wanafunzi kwamba Petro alikuwa mmoja wa wanafunzi wa Yesu na alikuwa amemkana Yesu wakati wa kusulubiwa kwake. Hata hivyo Yesu alikuwa amemsamehe na sasa alikuwa akiwaambia watu kwa ujasiri juu ya Yesu. Makosa yake hayakuwa mabaya sana kiasi cha kutoweza kusamehewa na sasa aliweza kutumiwa kwa nguvu kwa ajili ya Mungu. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mathayo aliitikia mara moja wito wa Mwokozi.<br>2. Mathayo aliacha kazi isiyo ya uaminifu ili kuwa mwanafunzi wa Bwana Yesu aliyeitika mara moja. Alikuwa mmoja wa wale wanafunzi kumi na wawili. ***(9: 9)***<br>3. Alipata heshima ya kuandikia Injili ya Mathayo na kuonyesha jinsi Yesu alivyo Mfalme aliyetarajiwa kwa muda mrefu ambaye Wayahudi wanamwita Masihi.<br>4. Eleza kwa kifupi maelezo ya Mathayo juu ya kuja kwa Bwana Yesu na sisitiza jinsi Mathayo anavyoelezea kwamba unabii mwingi wa Agano la Kale juu ya Bwana Yesu ulitimizwa alipokuja hapa duniani. ***(Mathayo 1 & 2)***<br>5. Mathayo anaandika nasaba ya Yesu, huduma Yake ya hadharani na kumalizia na majaribu Yake, kifo, maziko, na ufufuo - msingi wa wokovu wetu, na kusababisha kitabu chake kuitwa 'Injili'. Andika majina mawili kwenye karatasi. "Mfalme aliyeahidiwa kwa muda mrefu," na "Mfalme aliyekataliwa na kusulubiwa"<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Mathayo | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Petro, mmoja wa wanafunzi wa Yesu, alihubiri Habari Njema kwa wengi akielezea kwamba wanatakiwa kutubu dhambi zao na kumtumaini Kristo aliye hai. Wengi walikuja kuwa Wakristo na walimwamini Yesu Kristo kwa ajili ya wokovu - 3,000 waliongezeka zaidi ya wale 120 ambao walikuwa tayari Kanisani! Tafakari pamoja na wanafunzi jinsi gani jambo hili lilikuwa la ajabu kuona watu wengi sana wanakuwa Wakristo kwa muda mfupi sana. ***(2: 38-41)***<br>2. Hawa Wakristo wapya walianza kufanya kazi pamoja kama jamii - kanisa lilikuwa linaundwa. Waliungana na Wakristo wengine, walisikiliza mafundisho ya mitume, na walishiriki katika mikutano ya ushirika, ukumbusho wa kifo cha Yesu na katika sala. Eleza wanafunzi jinsi wanavyohitaji kuwa na watu ambao wanaweza kuwasaidia kujifunza Neno la Mungu, kuomba, na kukomaa katika imani yao. ***(Matendo 2: 42)***<br>3. Wakristo wote walikutana pamoja na kushirikishana mali zao. Hii haikumaanisha kuwa waligawiana kila kitu, lakini waligawa mali zao kwa wale walio na uhitaji, kama familia. Walitambua umuhimu wa kuwa ndugu na dada katika Kristo na kwamba maana yake ni kugawiana mali na kupendana katika Kristo. ***(Matendo 2: 42-47)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Wakristo kuwa pamoja. |
| REJELEA SOMO | Rejelea somo kwa kuuliza wanafunzi maswali ambayo yatawasaidia kujibu maswali yaliyoulizwa katika Somo la Kwanza. | Mkiwa wawili wawili, andaeni orodha ya njia zinazofaa ambazo Wakristo leo wanazitumia katika kukua na kukomaa katika imani yao, kama jamii. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kuamua kuitikia mara moja na kutoa maisha yetu kwa Bwana Yesu.<br>2. Kutambua vizuri kwamba Yesu hakuwa tu Mfalme wa Wayahudi bali pia ni Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana na, kwa hivyo, anastahili tumtumaini na kumtumikia.<br>3. Kuelewa kwamba Bwana Yesu hakuhitaji kujiokoa mwenyewe na ilikuwa lazima astahimili msalaba ili kuwaokoa wenye dhambi kama sisi. Nukuu yafuatayo kwa wanafunzi: *'Yeye mwenyewe hakuweza kujiokoa, Ilikuwa lazima afe msalabani, vinginevyo rehema haingeweza kuwafikia wenye dhambi walioharibiwa; Ndiyo, ilikuwa lazima Kristo Mwana wa Mungu amwage damu, ili watenda dhambi waweze kuwekwa huru mbali na dhambi. '*- Albert Midlane | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Ikiwa sisi ni Wakristo, je! Tunahakikisha kuwa tunakuwa na muda wa kuhusiana na Wakristo wengine, katika ushirika na katika kujifunza kila mmoja kwa mwenzake? Hatutakua kiroho kama hatujifunzi Neno la Mungu na kuomba pamoja.<br>2. Tunapaswa pia kufikiria juu ya jukumu letu la kusaidiana kwa kila njia inayowezekana, kama ndugu na dada katika Kristo. Familia ya Mungu inafanya kazi vizuri zaidi pale wanafamilia wake wanapofanya kazi pamoja.<br>3. Je! Unahisi kama umefanya makosa mengi kiasi cha kukosa sifa ya kumtumikia Yesu? Petro alikuwa amemkana Yesu, lakini bado alitumiwa kuwafikia maelfu ya watu kwa Habari Njema - Mungu anaweza kufanya vivyo hivyo kwa kutumia maisha yako! |

| | **B8 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Pili – Waandishi wa Injili**<br>**Mada – Marko** | **B8 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Pili – Njia iliyoko mbele**<br>**Mada – Ubatizo wa Kikristo** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 12: 5-12; Marko 1: 29-42***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Marko 10: 45***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Marko katika injili yake anamlenga Yesu kama 'Mtumishi Mkamilifu' na anaandika juu ya kile Alichofanya zaidi ya kile Alichosema.<br>2. Marko anaonyesha jinsi Bwana Yesu anavyowachagua wengine wamtumikie. | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 28: 16-20, Matendo 8: 34-39, 18: 8***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 2: 41***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ubatizo ni tendo la utii kwa Kristo.<br>2. Watu wengi katika Biblia wanakuwa Wakristo na kubatizwa kwa kuitikia imani yao.<br>3. Ubatizo ni ushahidi wa hadharani wa kumfuata Kristo. |
| **TOA UTANGULIZI** | Katika Injili ya Marko tuna habari ya Bwana Yesu akitoka Mbinguni kuja duniani sio kwa ajili ya kutumikiwa, bali kutumikia, na kutoa maisha yake katika msalaba wa Kalvari kuwa fidia ya wengi. (kama Mstari Muhimu) Wakati akiwa duniani, Bwana Yesu alikuwa mtiifu kabisa kwa mapenzi ya Mungu na matendo yake makuu yalifanywa kwa nguvu ya Roho Mtakatifu wa Mungu. Inafurahisha pia kuona kwamba Marko, mwandishi, ameanza vizuri, anapunguza bidii katika huduma kwa muda, lakini mwishowe anarejeshwa na kufaa katika huduma ***(2 Timotheo 4: 11)*** kwa ajili ya Bwana. | Uliza wanafunzi kama wamewahi kushiriki ibada ya ubatizo au wamewahi kubatizwa. Waombe washirikishe uzoefu wao; ilikuwaje. Nini kilitokea? Wanadhani ilikuwa inaashiria nini? |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Marko alitoka kwenye familia ambayo nyumba yao ilitumiwa na Wakristo huko Yerusalemu, ambao walikuwa wakimuombea Petro aachiliwe salama kutoka kwa Herode ambaye alikuwa amemuua Yakobo. ***(Matendo 12: 5-12)***<br>2. Marko alitaka kumtumikia Mungu katika kueneza Injili na ingawa alianza safari na Paulo na wenzake katika safari yao ya kwanza ya umishonari, aliwaacha na kurudi Yerusalemu. ***(Matendo 12:25, & 13: 13)***<br>3. Paulo alichukulia kujiondoa kwa Marko kama kasoro katika huduma na hakumruhusu Marko aandamane naye katika safari yake ya pili ya umishonari. ***(Matendo 15: 37-39)*** Hata hivyo, mwishowe Marko alirejezwa na kuaminiwa tena na Paulo, na akaendelea kumtumikia Bwana Yesu.<br>4. Ingawa Marko alikuwa ameshindwa katika huduma yake, aliandika kwa urefu sana katika Injili ya Marko, juu ya yale aliyofanya Bwana Yesu wakati akiwa hapa duniani, hasa miujiza Yake. Alijumuisha kuponywa kwa mama mkwe wa Simoni, kutakaswa kwa mwenye ukoma na kutuliza dhoruba wakati wanafunzi wakiwa kwenye mashua katika Bahari ya Galilaya.<br>5. Weka mkazo kuhusu vichwa viwili kwenye karatasi. "Marko anamuelezea Yesu kama Mtumishi Mkamilifu". "Marko anaonesha kwamba Bwana Yesu anawatumia wengine kumtumikia.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Marko | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Kabla Yesu hajaondoka duniani, aliwapa wanafunzi Agizo Kuu. Hapa ndipo alipowaambia waende ulimwenguni mwote na kufanya wanafunzi ulimwenguni kote na kuwabatiza kwa jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Yesu aliahidi kuwa pamoja nao wakati wanafanya hivi. Pia aliwapa mamlaka ya kufanya hivyo. ***(Mathayo 28: 18-20)***<br>2. Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi wabatize watu. Ubatizo unaunganisha waumini na Yesu Kristo katika kifo chao kwa dhambi na ufufuo wao kwa maisha mapya. Wanapata maisha mapya wanapokuwa Wakristo. Wanaacha maisha yao ya zamani, na kuanza upya, kwa sababu ya damu ambayo Yesu aliimwaga msalabani. Ubatizo unaonyesha hili hadharani kwa kila mtu. ***(Warumi 6: 3-7)***<br>3. Ubatizo pia unaashiria kujitiisha kwa Kristo, utayari wa kuishi katika namna anayopenda Mungu, na kujitambulisha kwa watu wenye agano na Mungu.<br>4. Katika habari kwenye ***Matendo 8***, Filipo anamwambia towashi Mwethiopia Habari Njema ya Yesu Kristo. Anakuwa Mkristo na mara moja anabatizwa.<br>5. Katika ***Matendo 18: 8***, Paulo, mtume, anawaongoza watu wengi kwa Yesu Kristo. Ubatizo unaonekana kufuata mara tu baada ya ukiri wao wa imani.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Ubatizo wa Kikristo. |
| **REJELEA SOMO** | Rejelea somo ukitumia maswali yafuatayo:<br>1. Marko anamuelezeaje Bwana Yesu katika Injili yote?<br>2. Marko alitoka katika familia ya aina gani? Kwa nini?<br>3. Marko alitaka kufanya nini katika maisha yake?<br>4. Ijapokuwa Marko alimkatisha tamaa Paulo katika safari ya kwanza ya umishonari, tunajuaje kwamba alirejezwa kikamilifu katika utumishi tena?<br>5. Taja kitendo fulani cha utumishi ambacho Yesu alikifanya wakati akiwa duniani. | Jifunze Agizo Kuu (Mathayo 28: 16-20)<br>1. Yesu anawezaje kuagiza mambo haya? (mstari wa 18)<br>2. Ni maagizo gani manne ambayo wanafunzi walipewa?<br>3. Je! Kuwa mwanafunzi kunamaanisha nini? Je! Ni mchakato unaoendelea?<br>4. Yesu anawaahidi nini ikiwa watafuata maagizo Yake? |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Taja kitendo cha utumishi tunachoweza kufanya katika kumtumikia Bwana Yesu.<br>2. Kusonga mbele katika utumishi Wake hata kama pengine tulishindwa hapo zamani.<br>3. Kumtumaini Yesu katika majaribu na dhoruba za maisha. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Umempa Yesu maisha yako na unatafuta kuishi kwa ajili yake katika maisha yako mapya?<br>2. Je, umebatizwa kwa kutii Neno Lake? Ikiwa sivyo, kwa nini? |

| | **B8 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Tatu – Waandishi wa Injili**<br>**Mada – Luka** | **B8 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Tatu – Njia iliyoko mbele**<br>**Mada – Meza ya Bwana** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 1: 1-4; Luka 4: 1-13***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 19: 10***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Luka anasisitiza kwamba pamoja na kuwa Mwana wa Mungu, Bwana Yesu alikuwa 'Mtu Mkamilifu'.<br>2. Majaribu yanathibitisha Bwana Yesu hakuweza kutenda dhambi na kwa sababu alikuwa mtu mtakatifu, asiye na dhambi, aliweza kuwa Mwokozi wa wenye dhambi. | **Neno la Biblia:** ***Marko 14: 22-25, 1 Wakorintho 11: 23-31***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Wakorintho 11: 26***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alituamuru tumkumbuke kwa namna ya kipekee.<br>2. Lazima tuuchukulie ukumbusho huu kwa uzito. |
| **TOA UTANGULIZI** | Ingawa Luka na Matendo aliandikiwa Theofilo, tunajua kidogo juu ya mtu huyo. Cheo chake 'mtukufu' ***(Luka 1: 3)*** kinaashiria alikuwa afisa wa serikali. Jina lake linamaanisha 'rafiki wa Mungu'. Labda alikuwa Mkristo mwenye kazi ya kuwajibika katika Dola ya Kirumi. Luka alimpa maelezo kwa maandishi kuhusu maisha ya Yesu ili kuondoa makosa yanayotokea pale maelezo yanapotolewa kwa mawasiliano ya mdomo. | Waulize wanafunzi wafikirie njia wanazotumia kumkumbuka mtu ambaye hayuko pamoja nao, pengine kwa picha, au kumbukumbu maalum. Yesu aliwaacha wanafunzi na njia maalum ya kumkumbuka wakati atakapokuwa hayupo nao tena. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Luka alikuwa daktari mkristo mmataifa ambaye alikuwa rafiki wa karibu sana na mtume Paulo. ***(Wakolosai 4: 14)***<br>2. Luka anamtaja Yesu katika kuzaliwa Kwake kuwa 'Mwokozi ambaye ni Kristo Bwana' ***(Luka 2: 11)***. Alikuwa Mungu aliyefanyika mwili.<br>3. Luka anaandika kwamba Yesu alikuwa mkamilifu kabisa katika ukuaji wake wa kawaida ***(Luka 2: 52)***. Kuongezeka kwa Bwana katika hekima ina maana ya ukuaji Wake wa kiakili, kuongezeka kwake kwa kimo ina maana ya ukuaji wake wa kimwili, ukuaji Wake 'wa kibali kwa Mungu' ina maana ya ukuaji Wake wa kiroho na 'wa kibali kwa wanadamu' ina maana ya ukuaji Wake wa kijamii.<br>4. Eleza kwa kifupi majaribu ya Yesu ***(Luka 4: 1-13)*** na uoneshe jinsi hili linavyodhihirisha kwamba alikuwa mkamilifu na hakuanguka katika majaribu.<br>5. Katika ***Luka 23***, tuna maelezo ya kifo cha Bwana na maoni mengine ya ajabu yalitolewa juu yake na Pilato, mmoja wa wale wezi na akida, kwamba wote walionyesha ukamilifu wa Bwana Yesu. ***(Luka 23: 14, 41 na 47)*** *Eleza kwamba ni jambo la muhimu kwamba Yesu hakuwa na dhambi; la sivyo hangekufa kwa ajili ya dhambi zetu. Leo huyu Mtu Mkamilifu yuko Mbinguni na anataka kuwaokoa wenye dhambi. Pia anawatunza walio wake na waliomtumaini kama Mwokozi na Bwana.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Luka | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Usiku wa mwisho wanafunzi na Yesu walikuwa pamoja, Yesu alichukua mkate na divai na akashukuru kwa ajili yao. Alisema kwamba mkate huo ni mwili Wake, uliomegwa kwa ajili yao na divai ilikuwa ni damu yake, iliyomwagika kwa ajili yao. Kisha akawaambia wale mkate na kunywa divai ili kumkumbuka. ***(Marko 14: 22-25)***<br>2. Wanafunzi hawakuelewa kwa ukamilifu, kwani ni Yesu tu ndiye alijua kitakachotokea siku za karibuni. Lakini wanafunzi walikumbuka agizo hili.<br>3. Hii ni njia maalum kwa Wakristo kufikiria na kutafakari juu ya kifo na mateso ya Bwana Yesu, kwa kula mkate na kunywa divai. ***(1 Wakorintho 11: 23-26)***<br>4. Kama vile Pasaka ilivyokuwa sherehe ya kutolewa kwa Israeli kutoka utumwani Misri, vivyo hivyo kula mkate na kunywa divai ilikuwa sherehe ya kutolewa kwetu kutoka dhambini kupitia kwa Kristo.<br>5. Bwana Yesu anawaambia wanafunzi wake kwamba wale mkate na kunywa divai tu mpaka atakaporudi. Huu haukuwa tu ukumbusho wa maisha na kifo cha Yesu bali pia kukumbushwa kuhusu ufalme wa Mungu ulioahidiwa!<br>6. Yesu alitaka kula chakula hiki cha Pasaka pamoja na wanafunzi wake kwa vile Yesu mwenyewe alipaswa kuwa Mwanakondoo wa kweli wa Pasaka, aliyetolewa sadaka kwa ajili ya dhambi za watu. Hii inaashiria kutolewa kwa mwili na damu yake kwa ajili ya wanafunzi. ***(1 Wakorintho 5: 7)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Meza ya Bwana. |
| **REJELEA SOMO** | Rejelea somo ukitumia maswali yafuatayo:<br>1. Maudhui ya Injili ya Luka ni nini?<br>2. Kazi ya Luka ilikuwa ni nini?<br>3. Kwa nini alimwandikia Theofilo?<br>4. Kuna umuhimu gani wa majina aliyopewa Yesu wakati wa kuzaliwa kwake 'Mwokozi ndiye Kristo Bwana'?<br>5. Kwa nini Luka anaandika kuhusu majaribu?<br>6. Soma ***Luka 23: 14, 41 na 4***7 na mjadili kile ambacho hawa watu walisema kuhusu 'Mtu Mkamilifu'. | Katika ***1 Wakorintho 11: 27-31***, anasema kwamba tunapaswa kujihoji kabla ya kula mkate na kunywa divai kwa ajili ya ukumbusho. Jadili kile mnachofikiria kuhusu maana ya jambo hili. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Unamtazamaje Bwana Yesu - kama 'Mtu Mkamilifu' au kama mtu mwingine yeyote?<br>2. Je! Umemwamini Mtu huyu Mkamilifu kama Mwokozi wako? Kama umefanya hivyo, je! Unawaambia wengine kuhusu Mtu huyu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Sisi, kama Wakristo, tunashiriki mkate na divai na kuzingatia kwa umakini kile ambacho vinawakilisha?<br>2. Je! Tunajua kuwa katika "agano jipya" hatupaswi kupitia kwa makuhani na dhabihu, bali tunaweza kwenda moja kwa moja kwa Mungu kwa sababu ya Yesu? |

| | B8 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Waandishi wa Injili<br>Mada – Yohana | B8 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Njia iliyoko mbele<br>Mada – Kukua kama Mkristo |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Yohana 20: 26-31***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 20: 31***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yohana anasisitiza kwamba Yesu ni 'Mwana wa Mungu'.<br>2. Bwana Yesu alitumia usemi 'mimi ndimi' mara nyingi na kwa kufanya hivyo alikuwa akidai usawa wake na Mungu kwa maana Mungu alijiita 'mimi niko' katika Agano la Kale. ***(Kutoka 3: 14-15)*** | **Neno la Biblia:** ***1 Petro 2: 1-3, 2 Petro 3: 18, Acts 17: 10-12***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Petro 2: 2***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Wakristo wanapaswa kukua kila siku katika imani yao.<br>2. Wakati wote kuna mengi ya kujifunza kuhusu neema na maarifa ya Mungu kwa kila mtu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Yohana anaanza Injili yake kwa kumtaja Yesu kama 'Neno'. ***(Yohana 1: 1)*** Maneno ndiyo njia ambayo sisi tunaelezea au kujieleza kwa wengine. Mungu amejidhihirisha kikamilifu kwa ulimwengu huu katika nafsi ya Mwanawe, Bwana Yesu Kristo, wakati Mwana wa Mungu alipokuwa Mwana wa Mtu, alizaliwa na bikira Maria huko Bethlehemu, zaidi ya miaka 2000 iliyopita. Kwa kutufia, Ametuonyesha ni jinsi gani Mungu anatupenda na kwa hivyo ndiye kielelezo cha mawazo ya Mungu kwetu. | Jadilini kama kikundi jinsi vitu vinavyokua mfano, wanyama, watoto wachanga, mimea, miti. Ni kitu gani kinahitajika ili vikue? Ni nini kinatokea ikiwa havipati kile ambacho vinakihitaji? |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yohana anamtaja Yesu kama 'Neno' ***(Yohana 1: 1)***<br>2. Yohana anajitaja mwenyewe kama 'mwanafunzi ambaye Yesu alimpenda.' ***(Yohana 20: 2)***<br>3. Katika Injili ya Yohana, 'mimi ndimi' ni jina la Mungu na Yesu alitaja sifa au wema wa Mungu kwa njia saba tofauti:<br>Mkate wa Uzima. ***(Yohana 6: 35, 41, 48, 51)***<br>Nuru ya Ulimwengu. ***(Yohana 8: 12, 9: 5)***<br>Mlango. ***(Yohana 10: 7, 9)***<br>Mchungaji Mwema. ***(Yohana 10: 11, 14)***<br>Ufufuo na Uzima. ***(Yohana 11: 25-26)***<br>Njia, Ukweli, na Uzima. ***(Yohana 14: 6)***<br>Mzabibu. ***(Yohana 15: 1, 5)***<br>4. Yohana aliandika Injili yake ili tuweze kumwamini Bwana Yesu na kupata uzima wa milele. ***(Yohana 20: 30-31)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Yohana | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Kama Mkristo, kuna namna fulani ambayo tunapaswa kuishi. Tunapaswa kuonyesha tabia ya Kristo katika mwenendo na matendo yetu. Kuna mistari mingi katika Biblia ambayo inatusaidia kujua jinsi tunavyopaswa kuishi kama tunataka kumheshimu.<br>2. Katika ***1 Petro 2: 1***, inatuambia kwamba hatupaswi kuwa wadanganyifu, wanafiki, na wenye wivu au kusema mambo mabaya.<br>3. ***1 Petro 2: 2*** - inazungumza juu ya Mkristo mpya kuwa kama mtoto mchanga. Ili kukua, lazima anywe maziwa. Maziwa haya ni Neno la Mungu. Ukuaji huu haukomi na kadiri mtoto mchanga anavyokua, bado anahitaji chakula. Vivyo hivyo, hakuna wakati wowote katika maisha ya Mkristo ambapo hawahitaji chakula (Biblia) katika kuwasaidia kukua.<br>4. ***2 Petro 3: 18*** inatufundisha kukua katika neema na maarifa ya Bwana wetu. Jadili na wanafunzi kuhusu maana ya neema na maarifa na jinsi gani tunaweza kukua katika hiyo neema na maarifa.<br>5. Wakati Paulo na Sila walipokuwa wakihubiri Injili, huko Beroya, watu walipendezwa sana na kufurahia kile walichokuwa wakisema. Katika ***Matendo 17***, inasema kwamba walikuwa wapokeaji makini, wasikilizaji wenye shauku, na walichunguza Maandiko kila siku. Walikuwa na bidii sana katika kujifunza ili wamjue Mungu zaidi!<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** – hakuna picha inayofaa. |
| **REJELEA SOMO** | Chukua kila moja katika sifa saba za 'Mimi ndimi' zilizoorodheshwa hapo juu na jadili jinsi kila moja inavyoonesha kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. | Watu wa Beroya ambao Paulo na Sila walizungumza nao ***(Matendo 17: 10-12)*** walikuwa na hamu ya kujifunza na kuchunguza Maandiko kuona kama Paulo na Sila walikuwa wakisema ukweli. Lazima tuwe waangalifu tusichukulie jambo fulani kuwa ni sahihi kwa sababu tu mhubiri au kiongozi anasema hivyo. Tunapaswa kujitafutia majibu kutoka kwenye Biblia. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Wape changamoto wanafunzi kusema kama wanaamini Yesu ni Mwana wa Mungu.<br>2. Ikiwa ni hivyo, je! Wamemwamini na kupokea uzima wa milele? ***(Yohana 1: 12-13, 5: 24)***<br>3. Ikiwa tumepokea uzima wa milele, tuko njiani kwenda Mbinguni na tunapaswa kusoma Biblia zetu kila siku ili kugundua mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yetu. Tunapaswa pia kuomba kila siku na kumshukuru Bwana Yesu kwa huruma zake kwetu na kumwomba atupe nguvu ya kuyatendea kazi yale tunayosoma katika Biblia. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Tunatafuta kukua kila siku? Je! Tunasoma na kuomba na kutaka kujifunza zaidi juu ya Mungu ili imani yetu iweze kuimarishwa? Tutakua pale tu tutakapojifunza Neno la Mungu na kuongozwa na Roho Mtakatifu.<br>2. Je! Tunawezaje kujilinganisha na watu wa Beroya? Je! Sisi tunawasikiliza kwa makini wale wanaotufundisha? Je! Tunachunguza Maandiko kila siku ili kupata majibu?<br>3. Jadili jinsi tunavyoweza kuwa na hakika kwamba Biblia ni Neno la Mungu. |

| | B9 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Kwanza – Musa<br>Mada – Mtoto kwenye kisafina | B9 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Kwanza – Musa<br>Mada – Mwana wa Mfalme |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 1: 6-20 na 22; 2: 1-10***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Waebrania 11: 23***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Waisraeli walikuwa wameongezeka sana kwa nguvu na idadi huko Misri kiasi kwamba Farao alifikiri watakuwa tishio kwake wakati wa vita, kwa hiyo aliamuru watoto wote wa kiume waangamizwe.<br>2. Mungu alipanga kumtumia Musa kumdhibiti Farao na kuwaokoa Waisraeli kutoka utumwani kwa hiyo alimhifadhi Musa akiwa mtoto mchanga asizamishwe katika Mto Nile. | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 1: 5-22; 2: 1-25***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Waebrania 11: 23***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Waisraeli walikuwa wameongeza sana kwa nguvu na idadi huko Misri kiasi kwamba Farao alifikiri watakuwa tishio kwake wakati wa vita, kwa hiyo aliamuru watoto wote wa kiume waangamizwe.<br>2. Mungu alikuwa na mpango juu ya maisha ya Musa – alitakiwa kuwatoa wana wa Israeli katika nchi ya Misri. |
| **TOA UTANGULIZI** | Rejelea Masomo B6 & B7 na waeleze wanafunzi kwamba miaka 300 baada ya Yusufu na ndugu zake kufika Misri Waisraeli walikuwa wameongezeka kwa idadi. Farao mpya alikuwa anatawala ambaye alikuwa amewafanya watumwa. Wakati huo huo, Mungu alikuwa akifanya mipango yake kwao katika kuzaliwa na kuhifadhiwa kwa Musa. Musa ndiye alitakiwa kuwaongoza kuingia katika nchi ya Kanaani. | Rejelea Mafunzo B6 & B7. Waeleze wanafunzi kwamba wakati Yusufu alipokufa, wana wa Israeli walikuwa wameshakuwa familia kubwa. Hata hivyo, wakawa taifa kubwa, ambalo lilimpa wasiwasi Farao mpya akawafanya watumwa. Lakini, Mungu hakuwasahau na aliandaa mpango wake kwa taifa la Israeli. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Farao aliingia madarakani na mafanikio ya Waisraeli ***(1: 7)*** yakageuka mateso ***(1: 8-11)*** lakini Mungu aliwatazama na kuwahifadhi. ***(1:12)***<br>2. Farao alitoa agizo kwamba watoto wa kiume wote wauawe wanapozaliwa tu kujaribu kuzuia idadi kuongezeka zaidi. ***(1: 15-20)***<br>3. Musa alizaliwa na Amramu na Yokebedi na baada ya kumlea kwa miezi mitatu, wakamweka kwenye kisafina kidogo cha manyasi ambacho kiliwekwa kando ya Mto Nile. ***(2: 1-3)***<br>4. Mungu aliokoa maisha ya Musa kwa kumtumia dada yake Miriamu, mama yake na binti Farao kufanya hivyo. ***(2: 4-9)***<br>5. Musa alipata kiwango cha juu cha elimu kwa sababu ya kuwa 'mwana wa binti Farao' ***(Matendo 7: 22)*** na pia alikuwa mrithi wa kiti cha enzi cha Misri.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Mtoto kwenye kisafina. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Farao aliogopa kwamba Waisraeli watatishia ufalme wake, kwa hiyo aliwafanya watumwa kujaribu kuzuia ukuaji wao. ***(1: 8-11)***<br>2. Waisraeli walizidi kuwa na nguvu zaidi, kwa hiyo Farao akawaamuru wakunga kuwaua watoto wote wa kiume wanaozaliwa lakini, kinyume na maagizo yake wakunga wakaokoa maisha yao. ***(1: 15-20)***<br>3. Musa alipozaliwa, kisafina kidogo kilitengenezwa, na mama yake akamweka ndani yake kando ya Mto Nile. ***(2: 1-3)***<br>4. Binti Farao alimwokoa Musa na mwishowe mama yake akawa mlezi wake. ***(2: 4-9)***<br>5. Musa alilelewa katika ikulu. Alipokuwa mtu mzima, alijaribu kuanza kuonyesha nguvu zake kwa kuwasaidia watumwa wa Israeli.<br>6. Anaua Mmisri ambaye alikuwa akimpiga mtumwa kisha analazimika kukimbilia nchi ya Midiani. ***(2: 11-15)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Mwana wa mfalme. |
| **REJELEA SOMO** | Waambie wanafunzi waandike kwa kifupi, kwa sentensi chache, wamejifunza nini kuhusu:<br>(i) Historia ya kuzaliwa kwa Musa<br>(ii) Kuokolewa kwake<br>(iii) Malezi yake<br>(iv) Elimu yake<br>(v) Cheo ambacho angeweza kukipata Misri | Rejelea somo hili kwa kuuliza maswali yanayohusiana kwa karibu sana na Funzo la Kwanza.<br>Fikiria juu ya jinsi ambavyo wakunga na wazazi wa Musa waliacha kutii sheria ya nchi. Muwe na majadiliano ya kikundi kama Wakristo wanapaswa kutii sheria ya nchi na kama kuna mazingira yoyote ambapo inakuwa vigumu kufanya hivyo. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Kama vile Mungu alivyodhibiti na kuongoza maisha ya mtoto, Musa, kwa sababu alikuwa na mpango mkubwa juu ya maisha yake, ndivyo atakavyodhibiti na kuongoza maisha yetu, tunapoweka imani yetu kwa Mwanawe, Bwana Yesu Kristo kwa ajili ya wokovu. Kwa hiyo tunajifunza kuwa Mungu anasimamia maisha yetu. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Wazazi wa Musa na wakunga walisimamia haki kwa sababu walimtumaini Mungu na kumcha, ingawa hali ilionekana kutokuwa na tumaini. Je! Tunaendelea kuwa wakweli kwake katika nyakati ngumu?<br>2. Dhambi ya Musa ilijulikana mara moja. Tunaweza kudhani kwamba tunaweza kuficha "dhambi ndogo", lakini siku zote zitagundulika, iwe ni kwa mtazamaji, au muhimu zaidi, kwa Mungu anayejua na kuona mambo yote. |

| | **B9 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Pili – Musa**<br>**Mada – Kosa lake kubwa** | **B9 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Pili – Musa**<br>**Mada – Mchungaji** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 2: 11-22***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Hesabu 32: 23***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Musa anataka kuanza kuwasaidia watu wake.<br>2. Hatuwezi kumficha Bwana Yesu dhambi zetu ingawa tunaweza kujaribu kuzificha kwa wengine.<br>3. Tunapotubu dhambi zetu na kuziungama kwa uaminifu mbele za Bwana Yesu, atatusamehe. (wakumbushe wanafunzi kuhusu ***1 Yohana 1: 9***) | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 3: 1-16; 4: 1-17***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 7: 35***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu anamtokea Musa na kumwambia arudi kuwaokoa watu Wake.<br>2. Mungu anaahidi kuwa pamoja na Musa katika kile alichomwitia kufanya. |
| **TOA UTANGULIZI** | Wakumbushe wanafunzi jinsi ambavyo mwishoni mwa Somo la Kwanza, Musa alikuwa amefanyika 'mtoto wa binti Farao' na alikuwa amekulia ikulu. Katika somo hili sasa ana umri wa miaka arobaini ***(Matendo 7: 23)*** na anajali sana kuhusu jinsi wana wa Israeli walivyotendewa wakati wakiwa Misri. Kuua kwake Mmisri ***(Kutoka 2: 12)*** kulifanywa kwa sababu ya ari, lakini alikuwa amekosea kwa kutenda dhambi ya mauaji. Mungu alipanga kumtumia Musa kuwaokoa watu wake, lakini alitakiwa kungojea miaka mingine arobaini kabla ya kuwa tayari kufanya kazi ya Mungu! | Waeleze wanafunzi kwamba Mlima Horebu katika ***Kutoka 3: 1*** ni Mlima Sinai na ni mahali muhimu sana katika maisha ya Musa. Katika ***Kutoka 3:12***, Mungu anamwambia Musa: 'Mtamwabudu Mungu kwenye mlima huu.' Mungu alizungumza na Musa kwenye mlima huu na kumpatia 'Amri Kumi.' ***(19: 1-20)*** |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Musa alisikitishwa sana na taabu za Waisraeli, lakini Mungu hakupendezwa na kitendo chake cha kumuua Mmisri kwa kufuata tu msukumo. Alipaswa kumuomba Mungu juu ya hali hiyo na kutafuta mwongozo Wake. ***(Kutoka 2: 12***<br>2. Musa alifikiri kwamba kwa mkono wake mwenyewe angewaokoa Waisraeli, lakini huu haukuwa mpango wa Mungu.<br>3. Dhambi yake ilipojulikana, alikimbilia nchi ya Midiani. ***(2:15)***<br>4. Kwenye kisima huko Midiani alikutana na mkewe wa baadaye Sipora ***(2: 21)*** na wakapata watoto wawili wa kiume. Mwana mmoja aliitwa Gershomu akimaanisha 'mgeni.' Jina hili lilielezea hisia za Musa za upweke alipokuwa katika nchi ya Midiani. Pia alikuwa na mtoto mwingine wa kiume aliyeitwa Eliezeri akimaanisha 'Mungu ndiye msaada wangu'. Musa alimshukuru Mungu kwa kumtoa kutoka kwa Farao ambaye alitaka kumuua kwa sababu alikuwa amemuua yule Mmisri.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kosa lake kubwa. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Musa alikuwa amekimbia kutoka Misri na sasa akawa anaishi na Wamidiani. ***(3: 1)***<br>2. Mungu alisema na Musa kutoka kwenye kijiti kinachowaka moto na Musa akavua viatu vyake kwa heshima. Mungu alipomwambia kwamba anamtaka aende kwa Farao kuwatoa Waisraeli Misri, Musa alizungumzia kutostahili kwake kwa kazi hiyo. ***(3: 10-11)***<br>3. Wakati Wamisri wakiwa na miungu mingi, Musa aliambiwa na Mungu awaambie Waisraeli 'Mimi niko amenituma kwenu' ***(3: 14)*** - Mungu pekee wa kweli na asiyebadilika!<br>4. Mungu anatumia fimbo ya Musa na kuibadilisha kuwa nyoka, kumwonyesha Musa nguvu Zake na kuonyesha jinsi Musa anavyoweza kuwaonesha watu nguvu hiyo hiyo ili wajue Mungu ni nani hasa. ***(4: 1-5)***<br>5. Mwishowe Mungu alikubali kumruhusu Haruni awe msemaji wa Musa na Musa alitakiwa kumwambia Haruni aseme nini kama Mungu alivyomwambia. ***(Kutoka 4: 16)***<br>6. Musa anaondoka kwenda Misri kuongea na Farao kuhusu kuwatoa Waisraeli Misri. Pengine hii ilikuwa changamoto kubwa zaidi maishani mwake.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Mchungaji. |
| **REJELEA SOMO** | Rejelea somo hili kwa kusoma ***Matendo 7: 23-29*** na uwaulize wanafunzi maswali yanayohusiana na yale waliyoulizwa katika Somo la Pili ili kuwasaidia kukamilisha somo. | Chora bango la Musa, lenye puto ya hotuba, kuonyesha visingizio Musa alivyotoa wakati Mungu alipomwambia arudi Misri kuwaokoa watu wa Israeli. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Umuhimu wa kumwuliza Bwana Yesu atuongoze, katika kumtumikia Yeye, na katika kufanya mambo sahihi kama anavyopenda na sio kwa kufuata mawazo yetu wenyewe.<br>2. Umuhimu wa kutokufunika dhambi zetu bali kuziungama kwa Bwana Yesu. Wakumbushe wanafunzi kuwa Mungu anajua yote; hakuna kitu kinachofanyika kwa siri. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Mungu aliyemtokea Musa ndiye Mungu yule yule anayeweza kuishi mioyoni mwetu na katika maisha yetu leo? Wape changamoto wanafunzi ili ujue kama Mungu anaishi mioyoni mwao na anatawala maisha yao<br>2. Kama Mungu atatuita, kama wafuasi wa Kristo, kufanya jambo fulani, atatusaidia kulikamilisha kama ilivyokuwa kwa Haruni, aliyekuwa akiongea kwa niaba ya Musa. |

| | B9 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Musa<br>Mada – Kijiti kinachowaka moto | B9 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Musa<br>Mada – Kiongozi |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 2: 23-25; 3: 1-10***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Kutoka 15: 11***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alijua kuwa wana wa Israeli walikuwa wanateswa kama watumwa na mfalme mpya wa Misri, lakini alikuwa na mpango wa kuwarudisha katika nchi ya Kanaani.<br>2. Mungu alimwita Musa awaongoze wana wa Israeli kutoka Misri kwenda Kanaani. | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 7: 1-25***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mithali 29: 1***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Nguvu ya Mungu ni kubwa kuliko ya mwanadamu au shirika lolote - Yeye ni 'mwenye nguvu zote' - Ana nguvu zote.<br>2. Watu wengine humwita Mungu wakati wa shida tu na kusahau anavyosema kuhusu maisha yao wakati mambo yanapoenda vizuri. |
| TOA UTANGULIZI | Jadili na wanafunzi hali ya sasa; Musa ameondoka Misri na yuko katika maisha yake mapya huko Midiani. Hana kusudi la kurudi Misri, hasa kwa vile Farao anataka kumuua. Waisraeli bado wanateseka sana huko Misri na wanamlilia Mungu awasaidie. Mungu anaanza kujibu ombi lao, kupitia kwa Musa. | Fikiria pamoja na wanafunzi jinsi Musa anavyokuwa anajisikia wakati huu, bila kujua atakabiliwa na nini huko Misri. Wakati tunapokuwa na wasiwasi kuhusu jambo fulani, wakati mwingine tunahitaji kuhakikishiwa kuhusu kile kinachotokea, au kwanini kinatokea, na ni nani anatusaidia. Mungu alifanya hivyo kwa Musa katika ***Kutoka 7: 1-5.*** |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Ujuzi wa Mungu kuhusu hali ya wana wa Israeli - Aliona, Alisikia, na Alijua huzuni zao. ***(2: 23-25)***<br>2. Mungu anasikia kilio chao na anajifunua kwa Musa katika Mlima Sinai, katika tukio la kijiti kinachowaka moto kwamba Yeye alikuwa nani na pia kuhusu utakatifu Wake.<br>3. Mungu anamwambia Musa kuhusu anavyowajali ***(mstari wa 7)*** wana wa Israeli, jinsi atakavyowaokoa kutoka kwa Farao ***(mstari wa 8)*** na kwamba atamtumia Musa awe ndiye mtu wa kuwatoa Misri. (mstari wa 10)<br>4. Wakumbushe wanafunzi kwamba marejeo ya kwanza katika Biblia kwa neno 'takatifu' yanapatikana katika ***Kutoka 3: 5*** na kwa kuvua viatu vyake Musa alikubali mahali aliposimama ni 'patakatifu'. Tunapaswa kumwendea Mungu wetu siku zote kwa uchaji na heshima.<br>5. Musa alijifunza kitu juu ya utakatifu wa Mungu, na nguvu Zake alipokutana na Mungu kwenye 'kijiti kinachowaka'.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kijito kinachowaka moto. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu alimfanya Musa kuwa mtu mwenye nguvu ('Nimekufanya uwe kama Mungu kwa Farao' ***(7: 1)*** - ambaye alistahili kusikilizwa, lakini Farao alikataa kujitiisha kwake.<br>2. Musa na Haruni walifanya kama Bwana alivyowaamuru na Haruni alipotupa fimbo yake mbele ya Farao, ikawa nyoka na wachawi wa Farao walipotupa fimbo zao pia zikawa nyoka lakini fimbo ya Haruni ikazimeza fimbo zao, ikionyesha nguvu ya Mungu inavyotenda kazi. ***(7: 8-12)***<br>3. Musa na Haruni walinyoosha fimbo juu ya Mto Nile, na mto ukageuka kuwa damu. Samaki wakafa; maji hayakuweza kutumika kwa kunywa, kilimo, kuoga wala kuvua samaki. ***(7: 20-21)***<br>4. Farao alipinga madai ya Musa ya kuwaachia watu waondoke.<br>5. Soma ***sura ya 8-10***, ili uone mapigo zaidi ambayo Mungu aliyatuma kumfanya Farao asikilize na kisha kuwaruhusu Waisraeli waondoke. Lakini moyo wake ulikuwa mgumu, na bado alikataa. Walakini kukataa kwa Farao kufuata maagizo kulithibitisha kuwa mpango wa mwisho wa Bwana siku zote unatimia.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kiongozi. |
| REJELEA SOMO | Rejelea somo hili kwa kuwaongoza wanafunzi kwenye ***Matendo 7: 30-35***. Waonyeshe wanafunzi jinsi Stefano alivyozungumza juu ya maisha ya Musa na pia alitaja tukio la kijiti kinachowaka moto. | Soma Mstari Muhimu na jadili pamoja na darasa jinsi unavyodhani unahusiana na funzo hili. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Lazima tukumbuke kuwa Mungu ni Mungu mtakatifu, na tunapaswa kumpa heshima anayostahili. Hatupaswi kamwe kulitaja bure jina lake kama watu wengi wanavyofanya leo.<br>2. Ingawa Mungu ni mtakatifu, amemtuma Mwanawe, Bwana Yesu Kristo, afe kwa ajili ya wenye dhambi na atatusamehe dhambi zetu zote, pamoja na zile za kutokumheshimu ambazo tunaweza kuwa tumetenda, ikiwa tutatubu na kumtumaini Mwanawe. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Soma ***Zaburi 105: 23-29*** na fikiria jinsi Mungu anavyodhibiti kila kitu. Fikiria maana yake katika ulimwengu wa leo.<br>2. Kubadilika kwa mto kuwa damu lilikuwa ni tukio la muujiza lakini Mungu anaweza kufanya tukio la muujiza mkubwa zaidi katika maisha yetu tunapomwamini Bwana Yesu na kazi yake msalabani. |

| | B9 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Musa<br>Mada – Kuleta ujumbe wa Mungu | B9 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Musa<br>Mada – Mkombozi |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 5: 1-9; 22-23; 6: 1-9***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Waebrania 10: 31***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Musa na Haruni walimwendea Farao kumwambia awaruhusu wana wa Israeli waondoke lakini Farao hakukubali ombi lao.<br>2. Bwana anamhakikishia Musa kwamba Farao ataruhusu wana wa Israeli waondoke kwa sababu atamlazimisha awaruhusu kuondoka. | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 11: 1-10; 12: 1-13 & 21-42***<br><br>**Mistari Muhimu:** ***Yohana 1: 29; 1 Wakorintho 5: 7***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alionyesha hukumu yake kwa Wamisri kwa kutotii kwao lakini alionyesha rehema Yake kwa Waisraeli kwa utii wao.<br>2. Mwana-Kondoo wa Pasaka alikuwa mfano wa kifo na ufufuo wa Bwana Yesu ambaye amebeba adhabu ya dhambi zetu kwa kifo chake msalabani. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waeleze wanafunzi kwamba ingawa Mungu alikuwa amemwagiza Musa arudi Misri, Musa aliogopa kuhusu kitakachotokea. Mungu aliahidi kuwa naye, lakini Musa hakujua jinsi Farao atakavyofanya atakapomwona tena. Kwa hiyo, Mungu alimwambia Musa aende na ndugu yake Haruni ili amsaidie. | Taifa lenye nguvu la Misri halingeweza kumzuia Mungu kutimiza ahadi zake kwa Ibrahimu na watu wa Israeli. Pigo hili la mwisho lilisababisha utumwa ufikie mwisho huko Misri. Waisraeli walipaswa kutii maneno ya Musa na ndipo wawe salama kutoka kwenye hukumu ya Mungu. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Alipoulizwa kuhusu kuwaruhusu wana wa Israeli waondoke, Farao kwa dharau anakataa kutii hitaji la Mungu lililoletwa kwake na Musa na Haruni. ***(5: 4)***<br>2. Farao alizidisha mzigo wa kazi kwa wana wa Israeli kwa kuwafanya pia wakusanye majani ya kutengenezea matofali. ***(5: 6-7)***<br>3. Musa aliongea na Bwana juu ya jambo hili na alimhakikishia kuwa atawakomboa wana wa Israeli kutoka Misri. ***(5: 22-23, na 6: 1)***<br>4. Katika ***Kutoka 6: 6-8***, Bwana alisema, 'Nita' mara 7 na akasema katika ***Kutoka 6: 2*** 'Mimi ni Bwana'. Alitaka Musa na Haruni waamini nguvu Zake na ahadi Zake. Mungu pia alihakikisha kwamba, muda mfupi baadaye, Farao anaziona nguvu zake kwa kupeleka adhabu (mapigo) 10 juu ya nchi ya Misri.<br>5. Musa anapeleka taarifa hii kwa watu wa Israeli, lakini wamekata tamaa sana na kuvunjika kutokana na utumwa wao na mateso hata wasiweze kuamini jambo hili. ***(6: 9)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kuleta ujumbe wa Mungu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Musa na Haruni walikuwa wamemwonya Farao kuhusu kile ambacho Mungu angefanya kama angeendelea kupuuza nguvu za miujiza ya Mungu kama inavyoonekana katika mapigo tisa yaliyotokea. ***(tazama Zaburi 105: 26-36)*** Onyo la mwisho linatolewa. ***(11: 4-6)***<br>2. Pasaka imeanzishwa, na Waisraeli wameagizwa kunyunyiza damu ya mwana-kondoo mkamilifu kwenye nguzo mbili za kando na kizingiti cha milango ya nyumba zao.<br>3. Eleza umuhimu wa mwana-kondoo; jinsi alivyokuwa dhabihu, mbadala wa kufa kwa mzaliwa wa kwanza katika kaya. Mnyama alipaswa kufa ili mzaliwa wa kwanza asife. ***(12: 1-7)***<br>4. Usiku wa manane, hatimaye pigo lilianguka, na kila mtoto ambaye ni mzaliwa wa kwanza wa Wamisri alikufa lakini watoto wa Israeli waliokolewa kwa sababu damu ya mwana-kondoo ilinyunyizwa kwenye miimo na vizingiti vya milango. ***(12: 29-30)***<br>5. Mwishowe Farao alikubali kuwaruhusu watu wa Israeli waondoke. Sasa Kutoka kwa Waisraeli Misri kunaanza baada ya miaka 430 huko Misri. Ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu katika ***Mwanzo 15: 13-14*** inatimizwa!<br><br>**Elezea Mistari Muhimu na jinsi inavyohusiana na Funzo hili. Wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Mkombozi. |
| **REJELEA SOMO** | Fikiria kile ambacho tayari Mungu amemwambia Musa na jinsi Musa alivyomjibu Mungu wakati Farao alipokataa moja kwa moja. Waisraeli walipowatazama Musa na Haruni na kuwalaumu, Musa kwa upande wake, alimtazama Mungu na kumlaumu kwa kile kinachotokea. Mungu ni mvumilivu na mwenye rehema hivyo akawaeleza tena kusudi lake na ahadi yake akisema; "Mimi ni Bwana". | Wape hamasa wanafunzi wafikirie jinsi Pasaka inavyowakilisha dhabihu ya damu isiyo na hatia kwa ajili ya Waisraeli. Fikiria pia jinsi ilivyo ishara ya dhabihu kubwa zaidi inayokuja. (Dhabihu ya Bwana Yesu ya damu isiyo na hatia kwa ajili yetu - Alikuwa Mwanakondoo wa Mungu) |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Mungu anataka tuelewe kwamba Yeye ni Mungu mwenye nguvu zote.<br>2. Mungu anataka tuelewe kuwa ni jambo baya sana kutomtii.<br>3. Mungu anataka tuelewe kwamba hata katika wakati mgumu tunaweza kumwamini Yeye. Lazima tukumbuke kwamba hatatuacha lakini wakati wote ana mpango kwa ajili yetu. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Tunatambua gharama kubwa ambayo ililipwa kutuokoa kwenye dhambi zetu? Kwamba Yesu alilipa gharama hii na kutukomboa kwa kufa msalabani?<br>2. Je! Tunamshukuru kwa kubeba dhambi zetu juu Yake na kutuwezesha kuwa na uhusiano mzuri na Mungu? Tunachopaswa kufanya ni kumwamini Yeye na kukubali karama yake ya uzima wa milele. |

| | **B10 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Kwanza – Musa**<br>**Mada – Mwanakondoo wa Pasaka** | **B10 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Kwanza – Musa**<br>**Mada – Kupitia Bahari ya Shamu** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 12: 1-14, 29-36 & 50-51***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Kutoka 12: 13***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alionyesha hukumu yake kwa Wamisri kwa kutotii kwao na rehema yake kwa Waisraeli kwa utii wao.<br>2. Yesu alikuwa dhabihu ya mwisho na ndiye Mkombozi wetu. | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 13: 17-22, 14: 1-31***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Kutoka 14: 13***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alikuwa pamoja na Waisraeli.<br>2. Waisraeli walitilia shaka ulinzi na msaada wa Mungu.<br>3. Mungu alithibitisha nguvu na upendo wake kwa watu wake kwa kuwaokoa kutoka kwa Wamisri kwa mara nyingine tena. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize wanafunzi wafikirie sikukuu kadhaa ambazo tunasherehekea na kwamba zinaashiria nini mfano. Krismasi, Pasaka. Eleza kwamba sikukuu inaweza kuwa ukumbusho muhimu wa kile Mungu alichotufanyia. Waulize kama wamewahi kusikia juu ya sikukuu iliyoadhimishwa katika imani ya Kiyahudi - Pasaka. Katika habari ya leo, tutajifunza juu ya Pasaka. | Waambie wanafunzi wawaze kama vile wanaenda safari ndefu kuelekea mahali ambapo hawajawahi kufika. Wangehitaji kitu (ramani) au mtu awaonyeshe njia. Hivi ndivyo ambavyo Waisraeli walihitaji kwa safari yao ndefu kwenda Nchi ya Ahadi. Mungu aliwaongoza katika safari yao kwa njia maalum. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Rejelea pamoja na wanafunzi kuhusu mapigo yaliyokuwa yametokea na uelezee kwamba hili la mwisho lilikuwa baya kuliko yote. Mungu alikuwa anataka kuonyesha kwamba alikuwa na nguvu zaidi ya Farao.<br>2. Mungu alitoa maelekezo maalum kwa Musa na Haruni juu ya nini cha kufanya. ***(mstari wa 1-14)***<br>3. Waisraeli walilazimika kumuua mwana-kondoo asiye na kasoro na kupaka damu yake juu ya miimo ya milango ili kuepukana na kifo.<br>4. Eleza umuhimu wa mwana-kondoo; jinsi alivyokuwa dhabihu, yaani mbadala wa kuchukua nafasi ya kifo cha mtoto wa kwanza wa kiume nyumbani.<br>5. Eleza kwamba Pasaka ni sikukuu ya Kiyahudi kwa heshima ya usiku ambao Bwana "alipita juu ya" nyumba za wale ambao walikuwa wametoa dhabihu ya mnyama. Mtoto wa kwanza wa kiume wa kila kaya ambayo haikuwa na damu mlangoni aliuawa.<br>6. Eleza maana ya Ukombozi; kununua / kuokoa kutoka utumwani. Katika Agano la Kale, Mungu alikubali matoleo ya wanyama kwa ajili ya mwenye dhambi. Yesu alipokuja, alitoa maisha yake makamilifu kwa ajili ya dhambi zetu. Yeye ndiye Mkombozi wetu - Alitukomboa kutoka katika nguvu ya dhambi na kuturudisha kwa Mungu. Dhabihu ya Yesu ilisababisha dhabihu ya wanyama isihitajike tena.<br>7. Mwishowe Farao alikubali kuwaruhusu Waisraeli waende zao - Bwana ametimiza ahadi yake kwao! ***(12: 31-32)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Mwanakondoo wa Pasaka. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu aliwaongoza Waisraeli kutoka Misri. Aliwaongoza kwa nguzo ya wingu wakati wa mchana na nguzo ya moto wakati wa usiku. Ndipo wakajua alikuwa pamoja nao akiwaongoza na kuwasaidia. ***(13: 21-22)*** *Jadili na wanafunzi kwamba wakati mwingine watu wanataka ishara zinazoonekana kama hii kujua kwamba Mungu yuko pamoja nao. Lakini Mungu yuko pamoja nasi sasa na anatuongoza kupitia Biblia na kupitia Roho Mtakatifu - ikiwa tunamtumaini.*<br>2. Fikiria juu ya faraja ambayo Waisraeli walikuwa wanahisi walipotoka Misri. Walakini fikiria juu ya jinsi faraja hii ilivyogeuka kuwa woga wakati waliposikia kwamba jeshi la Farao lilikuwa likiwafuata ili kuwarudisha! ***(14:10)***<br>3. Waisraeli walianza kuogopa na kuanza kumlaumu Mungu kwa hili na kukasirika. Lakini Musa aliwakumbusha watulie. Mungu atawapigania. Musa alikuwa anajifunza kumtumaini Mungu. ***(14: 13-14)***<br>4. Mungu aliwaambia watu waendelee mbele na anawapatia njia ya kuokoka kupitia Bahari ya Shamu. Kisha Mungu akasababisha jeshi la Misri kuzama. Akafungua njia ya kuwaokoa watu wake. Mungu aliweza kufanya muujiza huu kwa kugawanya bahari ili kuonyesha kwamba watu wake hawahitaji nguvu zake tu bali pia upendo Wake. ***(14: 21-28)***<br>5. Waisraeli walimcha Mungu na kumwamini Mungu pamoja na Musa siku ile. ***(14: 31)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kupitia Bahari ya Shamu. |
| **REJELEA SOMO** | Baada ya miaka mingi ya utumwa na kumlilia Mungu, baada ya mapigo mengi na kukataa kwa Farao kumsikiliza Mungu, watu wa Israeli hatimaye wakawa huru! Jadilini kama kikundi jinsi walivyokuwa wanajisikia wakati wakitoka Misri. | Wape wanafunzi jaribio la funzo la leo kama njia ya kutathmini somo. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Tunatambua gharama kubwa ambayo ililipwa ili kutuokoa kutoka kwenye dhambi zetu? Kwamba Yesu alilipia gharama hii na kutukomboa kwa kufa msalabani?<br>2. Je! Tunamshukuru kwa kuzibeba dhambi zetu juu yake na kutuwezesha kuwa na uhusiano mzuri na Mungu? Tunachopaswa kufanya ni kumwamini Yeye na kupokea zawadi yake ya uzima wa milele. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Wakati mambo yanapokuwa hayaendi kama tunavyotaka au jinsi tunavyotarajia yaende, tunachukuliaje? Je! Tunamlaumu Mungu na kumkasirikia? Au je! Tunakabiliana na shida hizi kwa ujasiri kwamba Mungu atatusaidia kama tunamtumaini, hata kama sio katika namna ambayo tungetarajia?<br>2. Zingatia kutoka kwenye funzo hili kwamba Mungu ni Mungu wa yasiyowezekana. ***(Angalia Isaya 43: 2-3)*** |

| | **B10 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Pili – Musa**<br>**Mada – Bahari ya Shamu** | **B10 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Pili – Musa**<br>**Mada – Juu ya Mlima Sinai** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 13: 20-22, 14: 5-15, 19-31***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Kutoka 14: 14***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu aliwaokoa wateule wake kutoka Misri.<br>2. Waisraeli walianza kumtilia shaka Mungu na uangalizi wake kwao.<br>3. Mungu alikuwa pamoja nao, akiwaongoza na kuwalinda | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 19: 1-13, 16-25, 20: 1-21***<br><br>**Mistari Muhimu:** ***Kutoka 19: 5 & 20: 20***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu ni mtakatifu na mwenye nguvu.<br>2. Tuna fursa ya kuweza kumfikia Mungu kwa urahisi, jambo ambalo Waisraeli hawakuweza kulifanya.<br>3. Mungu aliwapa Waisraeli maelekezo kuhusu jinsi ya kuishi. |
| **TOA UTANGULIZI** | Fikiria jinsi ambavyo Waisraeli walikuwa wanajisikia. Kama taifa walikuwa wametumia miaka 430 Misri katika utumwa na sasa wanakuwa huru. Uliza wanafunzi kwamba wanadhani Waisraeli walikuwa wanafikiria nini wakati huu. | Fikiria kuhusu hali za kila siku tukiwa tuna kanuni na miongozo k.v. mwongozo wa jinsi ya kutumia kifaa, maelekezo ya namna ya kupika kitu fulani. Miongozo hii kwa kawaida iko ili kutusaidia. Ndivyo ilivyokuwa kwa Amri Kumi ambazo Musa alipokea kutoka kwa Mungu kwa ajili ya watu wa Israeli. Zilikuwepo kwa faida yao kuwaongoza katika maisha yao. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Hatimaye Waisraeli wakawa huru na kusafiri kuelekea Nchi ya Ahadi mbali na Misri! Fikiria jinsi walivyokuwa na furaha baada ya kuwa huru kutoka utumwani!<br>2. Mungu aliwaongoza Waisraeli kwa nguzo ya wingu mchana na nguzo ya moto usiku. ***(13: 21-22)*** Hii iliwaonyesha kuwa Mungu alikuwa pamoja nao wakati wote na alikuwa akiwaongoza. *Mara nyingi, tunatamani tungekuwa na ishara za kimwili kwamba Mungu yuko nasi leo. Lakini anaweza kutuongoza na kutusaidia kupitia Biblia na kupitia Roho Mtakatifu.*<br>3. Jeshi la Farao lilipoanza kuwafuata Waisraeli, Waisraeli waliingiwa na hofu na kulalamika kwamba Mungu hakuwajali. Hawakumtumaini. ***(14: 10-11)*** Walikuwa wamesahau kabisa jinsi Mungu alivyokuwa amewasaidia na kuwafikisha hapo walipofika. *Eleza kwamba mara nyingi tunaweza kuwa na mtazamo huu wakati mambo yanapokwenda vibaya katika maisha yetu.*<br>4. Musa alitulia na kuwa na tumaini katika hali hiyo, akiwakumbusha watu kwamba Mungu angewapigania. ***(14:14)***<br>5. Mungu alionyesha nguvu zake kuu kwa kuigawa Bahari ya Shamu ili Waisraeli wapite na kisha kuliangamiza jeshi la Wamisri baharini mara tu Waisraeli walipofika upande wa pili. ***(14: 21-22, 26-28)***<br>6. Waisraeli walimwogopa Bwana na kumtumaini na walimwamini Musa pia kama kiongozi wao. ***(14: 31)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Bahari ya Shamu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Imepita miezi miwili tangu Mungu awatoe Waisraeli Misri. Sasa anawaandaa kwa jambo linalofuata. ***(19: 1)***<br>2. Mungu anamwambia Musa awaambie watu jinsi walivyo wateule wake na jinsi watakavyokuwa mali yake ya kuthaminiwa. ***(19: 5-6)*** Anawaambia wajiweke wakfu. *Eleza maana ya kuweka wakfu - kutenga, kuandaa kimwili na kiroho ili kukutana na Mungu.*<br>3. Waisraeli hawakuweza hata kugusa mlima kwa sababu ulikuwa mtakatifu. Uwezo na utakatifu wa Mungu ulidhihirika kwa nguvu sana kiasi kwamba watu hawakuweza kumkaribia. ***(19: 10-13)*** *Tafakari jinsi inavyoshangaza kwamba sasa tunaweza kumkaribia huyu Mungu mtakatifu, mwenye nguvu kwa uhuru kwa sababu ya yote ambayo Bwana Yesu amefanya.*<br>4. Mungu anamruhusu Musa peke yake amkaribie na anampatia Amri Kumi. ***(20: 1-17)*** Sheria hizi zinawapa watu wa Waisraeli majukumu kwa Mungu na kila mmoja kwa mwenzake. Zilitolewa ili kuongoza Israeli kwenye maisha ya utakatifu wa vitendo na kuwawezesha kuona asili ya Mungu na mpango wa jinsi ya kuishi maisha yao.<br>5. Watu waliogopa na hawakuwa tayari kupanda mlima wenyewe, kwa hiyo Musa akatenda kazi kama mpatanishi kati yao na Mungu. Aliye mkuu kuliko Musa, Yesu, anakuwa Mpatanishi pekee kati ya Mungu na wanadamu. ***(1 Timotheo 2: 5)***<br>6. Musa anawaambia wasiogope lakini hofu ya Bwana iwe pamoja nao. Hofu yao ilikuwa woga. Musa alitaka kwamba badala ya wao kuwa na woga wawe na hofu ya Bwana ambayo inaleta uaminifu na utii na kuwafanya wasitende dhambi. ***(20:20)***<br><br>**Elezea Mistari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Juu ya Mlima Sinai. |
| **REJELEA SOMO** | Tunga kichekesho cha habari hii; Mungu akiwaongoza Waisraeli, Waisraeli wanagundua Wamisri wanawafuata na kisha jinsi Mungu anavyowaokoa. | Rejelea somo kwa kuwauliza wanafunzi waorodheshe Amri Kumi na kujadili kila moja. Jinsi gani Amri zinaweze kutendewa kazi katika maisha yetu sisi wenyewe? |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Wakati mambo mabaya yanapotokea katika maisha yetu, je! Tunamlaumu Mungu na kusema kwamba ni kwa sababu hayupo au hayuko tayari kutusaidia? Au je! Tunaamini kama Musa kwamba ametusaidia na ataendelea kutusaidia na kutupigania, tunapomtumaini Yeye peke yake? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Tunapofikiria jinsi Waisraeli walivyoogopa na jinsi walivyokuwa hawastahili kuingia kwenye uwepo wa Mungu, je! Tunafahamu kweli kuwa ni fursa kuwa na uwezo wa kukaribia uwepo wa Mungu kwa uhuru, kwa sababu ya Yesu Kristo? Tunapaswa kumshukuru kwa kuchukua dhambi zetu juu yake ili tuwe watakatifu mbele za Mungu. ***(Angalia 2 Wakorintho 5: 21)*** |

| | **B10 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Tatu – Musa**<br>**Mada – Safari ngumu** | **B10 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Tatu – Musa**<br>**Mada – Kutoka kwenye moto** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 17: 1-16***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Petro 5: 7***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Waisraeli wanaendelea kumtilia shaka Mungu.<br>2. Mungu hawaachi kamwe na anaendelea kuwapatia mahitaji yao na kuwapigania. | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 32: 1-35***<br><br>**Mistari Muhimu:** ***Kutoka 32: 26 & 33***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Baada ya muda mfupi watu wa Israeli walisahau Amri za Mungu.<br>2. Mungu aliwaonyesha rehema wale waliomfuata na kuwaadhibu wale ambao hawakumfuata. |
| **TOA UTANGULIZI** | Kumbuka jinsi Waisraeli walivyotoka mbali na jinsi Mungu alivyowapa mahitaji yao, alivyoleta mapigo huko Misri na kugawanyika kwa Bahari ya Shamu. Waulize wanafunzi wafikirie juu ya jinsi Waisraeli walivyojisikia kuhusu Mungu wakati huu. | Waambie wanafunzi wafikirie juu ya wakati ambapo walijua walikuwa wakifanya jambo ambalo ni baya. Fikiria ni kwanini mara nyingi tumesema ndiyo na kufuata mkumbo katika hali hizi. Katika funzo hili tunajifunza kwamba hatupaswi kuwa kama Haruni lakini kama Musa na kufuata njia za Mungu. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Waisraeli walikuwa wanaendelea tena, wakifuata maagizo ya Bwana. Lakini hakuna maji ya kunywa katika safari yao. Kwa hiyo, wanaanza kulalamika tena. ***(17: 2-3)*** Walilalamika kwa Musa badala ya kumwomba Mungu na kumtumaini.<br>2. Mungu anatenda kwa neema, licha ya manung’uniko yao, na kuwapatia maji kutoka kwenye mwamba - Hawaachi na anatenda muujiza! ***(17: 5-6)***<br>3. Matatizo yao hayajaisha kwani Waamaleki wanawashambulia! ***(17: 8)*** Kundi hili lilijulikana kama watu waovu na hatari ambao waliua kwa kujifurahisha. *Fikiria jinsi Waisraeli walivyokuwa wakijisikia baada ya kutoka Misri na matatizo yote waliyopata na sasa kukabiliwa na kuuawa na Waamaleki!*<br>4. Lakini Mungu aliwasaidia. Musa anasimama juu ya kilele na kuinua fimbo ya Mungu juu ya kichwa chake. Ilipokuwa juu ya kichwa chake, walikuwa wakishinda, lakini ilipokuwa chini ya kichwa chake, walikuwa wanashindwa! Mara mikono ya Musa ikawa imechoka kwa hiyo Haruni na Huri wakamsaidia kuinua mikono yake juu ya kichwa chake. ***(17: 11-13)***<br>5. Waisraeli walishinda vita siku hiyo - ni wazi kwamba Mungu alikuwa pamoja nao akiwasaidia kumshinda adui huyu. Hii pia ilionyesha kuwa Mungu atawaongoza watu wa Israeli kupitia kwa Musa.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Safari ngumu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Watu wa Israeli walipoteza subira ya kumngojea Musa ashuke kutoka Mlima Sinai. Walijiamulia wenyewe na kutaka kujitengenezea mungu wao. Walichagua sanamu ya uongo ambayo wangeweza kuidhibiti badala ya uongozi wa Bwana. Fikiria jinsi jambo hili lilivyokuwa likivunja Amri mbili za kwanza. ***(32: 1-4)***<br>2. Mungu alipoona kile kinachotokea, alikuwa tayari kuharibu taifa lote kwa sababu ya uasi wao ***(32: 10)*** lakini Musa alimsihi Mungu asifanye hivi. Mungu anaonyesha rehema hapa. ***(32: 11-14)*** Eleza maana ya rehema (kuepushwa na adhabu ambayo mtu anastahili).<br>3. Musa alirudi chini ya mlima na aliwakasirikia sana watu kiasi kwamba alizivunja mbao za Amri Kumi mbele yao, kuwaonyesha kuwa walikuwa wamevunja sheria za Mungu. ***(32: 19)*** Mungu naye aliwakasirikia zaidi watu.<br>4. Musa alikatishwa tamaa na Haruni kwa kupotosha watu wa Israeli. Alipaswa kujua kwamba kile watu wa Israeli walichokuwa wakifanya kilikuwa kibaya lakini badala yake alisikiliza malalamiko yao na kuwasaidia kutengeneza ndama huyu wa dhahabu ili wamuabudu. ***(32: 21-22)***<br>5. Musa anawauliza Waisraeli "Ni nani aliye upande wa Bwana?" Yeyote ambaye hakujibu na kumfuata Mungu, aliuawa siku hiyo. ***(32: 26-29)*** Utiifu kwa Mungu ni muhimu zaidi kuliko utiifu mwingine wowote.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kutoka kwenye moto. |
| **REJELEA SOMO** | Jifunze Mstari Muhimu na jadili na kikundi jinsi wanavyoweza kuutumia. Kumbuka kwamba Mungu anataka tumtumainie wakati wote. | Tafuta ***1 Yohana 5:21*** na ufikirie ni aina gani ya "sanamu" zinaweza kuchukua nafasi ya Mungu mioyoni mwetu. Tumia mstari huu na hizi "sanamu" kutengeneza bango la ukuta, ukionyesha umuhimu wa kumfuata na kumtii Mungu. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Wakati mwingine tunasahau kuwa Mungu anaweza kutusaidia katika hali ngumu? Lazima tukumbuke kumgeukia ili atusaidie kupigana vita zetu na kutusaidia katika hali zote ngumu.<br>2. Fikiria jinsi Haruni na Huri walivyomsaidia Musa kuinua mikono yake juu ya kichwa chake - walimtia moyo na kumsaidia. Tunawezaje kufanana hivi leo kwa kuwasaidia wengine? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Mara nyingi tunaweza kufanya makosa na kuacha kumtii Mungu. Lakini tunaweza kupokea msamaha kutoka kwa Mungu kwa kutubu na kwa kumuomba.<br>2. Haruni hakusimamia kile alichojua kiko sahihi. Je! Tunaweza kukumbuka nyakati katika maisha yetu ambapo tunafanya hivi na kufuata tu mkumbo? Omba kwamba Mungu atusaidie kumtii na tusianguke katika majaribu yanapotupata. |

| | B10 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Musa<br>Mada – Nyoka wa shaba | B10 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Musa<br>Mada – Jangwani |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Hesabu 21: 4-9, Yohana 3: 1-2 & 14-16***<br><br>**Mistari Muhimu:** ***Yohana 3: 14-15***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Waisraeli walimnung'unikia Mungu tena.<br>2. Ilibidi Mungu awaadhibu - BALI alifanya njia kwa ajili yao kuokolewa kutoka kwenye adhabu yao.<br>3. Hii ni picha ya matukio ya baadaye ambapo Yesu aliinuliwa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. | **Neno la Biblia:** ***Hesabu 21: 1-9***<br><br>**Mistari Muhimu:** ***Yohana 3: 14 & 15***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Waisraeli walisahau haraka sana jinsi Mungu alivyokuwa amewajali na kuwapa mahitaji yao hadi wakati huo.<br>2. Ilibidi Mungu awaonyeshe watu wa Israeli jinsi walivyokuwa wanatenda dhambi na kutomtumaini.<br>3. Mungu aliwapa njia ya kuepuka adhabu yao. |
| TOA UTANGULIZI | Waambie wanafunzi wafikirie kuhusu wakati ambao walikosa subira ya kungojea kitu au kungojea ahadi kutoka kwa mtu fulani. Eleza kwamba Mungu alikuwa tayari amewaahidi Waisraeli Nchi ya Ahadi, lakini walikuwa wakikosa subira ya kufika huko. | Fikiria kuhusu kusafiri safari ndefu. Mara nyingi, watu wanaweza kukosa subira na kuchoshwa na safari, hasa watoto. Wakati mwingine, wanataka kufika wanapokwenda mara moja. Hivi ndivyo Waisraeli walivyohisi juu ya kufika Nchi ya Ahadi ambayo Mungu alikuwa amewaambia habari zake. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Waisraeli wamekuwa jangwani sasa kwa karibu miaka 40 na wamekuwa wakivunjika moyo. Wakaanza kumnung'unikia Mungu tena - "Kwa nini umetutoa Misri ili tufe hapa ?!" ***(Hesabu 21: 4)***<br>2. Kwa hiyo, Mungu anakasirishwa na upungufu wao wa imani kwake. Anatuma nyoka wenye sumu kati yao na wengi wanakufa. Lakini Musa alimwomba Mungu kwa niaba ya watu kwa ajili ya msamaha. ***(21: 7)***<br>3. Mungu alimwambia Musa atengeneze nyoka wa shaba na kumweka juu ya mti na mtu yeyote aliyemtazama nyoka huyu alipona. Nyoka wa shaba aliwezesha Waisraeli kuponywa. Kwa kumtazama, Waisraeli walikuwa wakikiri kwamba hukumu hii ilitoka kwa Mungu na kwamba ni Mungu tu ndiye angeweza kuwaokoa kutoka kwa nyoka hao. ***(21: 9)***<br>4. Waisraeli walikuwa hawajajua hili bado lakini nyoka huyu juu ya mti alikuwa na maana kubwa. Katika ***Yohana 3,*** Yesu anaelezea kwamba kama vile Waisraeli walivyoponywa kwa kumtazama nyoka huyu, vivyo hivyo leo tunaweza kuponywa kutoka kwenye dhambi zetu kwa kutazama kifo cha Yesu alipoinuliwa msalabani. Sio nyoka aliwaponya Waisraeli bali imani yao ndiyo iliweza kuwaponya.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Nyoka wa shaba. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Waisraeli walikuwa wakizunguka jangwani kwa karibu miaka 40 na walikuwa wakikosa subira. Mungu alikuwa amewaahidi Nchi ya Ahadi, lakini ilikuwa haionekani popote bado. Kwa hiyo, walinung'unika na kumlalamikia Mungu kwa ajili ya hali yao, badala ya kukumbuka jinsi Mungu alivyowatoa mbali. ***(Hesabu 21: 4-6)***<br>2. Kabla ya hapo, walikuwa katika hali nyingi za hatari, lakini Bwana alikuwa amewasaidia na alipatikana kwa ajili yao, licha ya upungufu wao wa imani na kuendelea kunung'unika.<br>3. Lakini Bwana alikuwa amechoshwa na hali hiyo kwa hiyo akatuma nyoka wenye sumu, ambao waliwauma watu, na wengi wakafa. ***(21: 6)***<br>4. Mara watu wakatambua dhambi yao na kumwendea Musa amwombe Mungu msamaha. ***(21: 7)***<br>5. Kwa hiyo, Mungu alielekeza nyoka wa shaba awekwe juu ya mti na wale watakaomtazama wataishi. Kwa kumtazama nyoka huyu, walikiri kwamba Mungu alikuwa ametuma hukumu hii na ni Mungu tu ndiye anayeweza kuiondoa na kuwaokoa. ***(21: 9)***<br>6. Watu wa Israeli hawakutambua hilo, lakini hii ilikuwa ishara ya Bwana Yesu pale msalabani. Wale ambao walimtazama nyoka walipona maumivu yao na hawakufa. Vivyo hivyo, wale wanaomtazama Bwana Yesu msalabani na kumtumainia hawatakufa bali watapata uzima wa milele. (Tazama Mistari muhimu)<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Jangwani. |
| REJELEA SOMO | Waambie wanafunzi waangalie mstari unaojulikana sana, ***Yohana 3: 16*** na watafakari maana ya uzima wa milele. Watu wengi hawapendi wazo la uzima wa milele kwa sababu hawapendi maisha yao ya hapa duniani. Lakini uzima wa milele ambao Yesu anatoa hauna ugonjwa, kifo, uovu au dhambi! Tunapomjua Kristo na kumfuata, mtazamo wetu juu ya maisha haya ya hapa duniani unabadilika. | Mkiwa katika vikundi vidogo, tafuteni na kujifunza ***Zaburi 78: 10-38*** na kuorodhesha maajabu yote ambayo Mungu aliwafanyia watu wake na mtazamo wao kwake na kile alichokuwa amefanya. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Waisraeli walimnung'unikia Mungu kwa sababu hawakumtumaini, hawakutii sheria yake na walisahau yote ambayo alikuwa tayari amewafanyia. Fikiria jinsi mambo ambayo tunanung'unikia mara nyingi yanavyosababishwa na matendo yetu na mitazamo yetu. Tunapaswa kushughulikia manung'uniko yetu na tusiruhusu yatawale maisha yetu. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Watu wa Israeli walimnung'unikia Mungu juu ya hali yao ya sasa, ingawa hakuwa amewaacha hadi wakati huu. Mara nyingi, tunaweza kuwa hivi na kusahau baraka nyingi ambazo Mungu anatupatia na jinsi atakavyotutunza tunapomtumaini. Je! Tumemtazama Yesu msalabani, tukamtumaini, ili tuweze kuokolewa kutoka kwenye dhambi zetu, na kupata uzima wa milele? |

| | **B11 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Kwanza – Musa**<br>**Mada – Kukutana na Mungu** | **B11 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Kwanza – Sheria**<br>**Mada – “Mungu Mmoja”** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 19: 1-14***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Petro 1: 16***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu ni mtakatifu na mkamilifu.<br>2. Utii ni muhimu sana katika uhusiano wetu na Mungu.<br>3. Sheria za Mungu zinafunua dhambi za watu wake. | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 19: 16-25, & 20: 1-7, Mathayo 22: 34-40***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 22: 37***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu ni Mungu mtakatifu.<br>2. Mungu ni Mungu mwenye nguvu.<br>3. Mungu ni Mungu mwenye wivu.<br>4. Mungu ni Mungu mwenye upendo. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waambie wanafunzi wafikirie juu ya kile wanachofanya wanapoenda kwenye harusi Mfano kufua nguo zao, kuoga, na kuhakikisha wanaonekana wasafi sana na kuvaa vizuri kwa ajili ya siku kuu! Eleza jinsi watu wa Israeli walivyopaswa kufanya hivyo ili kujiandaa kukutana na Mungu, kwa sababu Yeye ni mkamilifu na hana dhambi na watu wa Israeli walikuwa wamefanya dhambi mara nyingi. | Katika funzo hili, tutatafakari jinsi Mungu alivyoamuru watu wa Israeli wasiwe na miungu mingine au sanamu isipokuwa Yeye. Ikiwa chochote kinaingia kati yetu na Mungu, basi kitu hicho ni sanamu. Fikiria mifano ya sanamu au miungu katika jamii ya leo na jadili pamoja na wanafunzi jinsi zinavyoweza kuchukua nafasi ya Mungu katika maisha yetu. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Musa tu ndiye aliyeweza kupanda mlimani ili kukutana na Mungu. Uwepo wa Mungu ulikuwa na nguvu sana na mtakatifu sana kiasi kwamba watu wa Israeli hawakuweza kupanda ili kukutana Naye. ***(mstari wa 3)***<br>2. Mungu alikuwa na sababu ya kuwakomboa Waisraeli kutoka utumwani Misri na sasa anawaambia. Anawataka wamtii na kumfuata. Mungu alitaka Waisraeli wawe taifa takatifu, watu wake maalum aliowachagua. ***(mstari wa 5-6)***<br>3. Waliposikia amri za Bwana watu waliitika kwa kusema kwamba watafanya kila kitu alichosema Bwana. ***(mstari wa 8)***<br>4. Mungu alimwambia Musa akawatakase watu wa Israeli kwa ajili ya ibada. ***(mstari wa 10)*** Hii ilikuwa kwa ajili ya kuwafanya wawe tayari kukutana na Mungu. Walitakiwa kuoga na kuandaa mioyo na akili zao ili kukutana na Mungu. Waeleze wanafunzi jinsi ambavyo kujisafisha wenyewe kimwili kungewasaidia pia kujaribu kuwa safi kiakili kwa ajili ya kumwabudu Mungu.<br>5. Soma Mstari Muhimu ili uone ni kwa nini walitakiwa kujiandaa kukutana na Mungu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kukutana na Mungu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Waisraeli walikuwa wameletwa kwenye Mlima Sinai na walikuwa wakiandaliwa na kutayarishwa kwenda kukutana na Mungu. Mungu alikuwa mtakatifu sana kiasi kwamba ilibidi wajaribu kujisafisha kwa nje kadri wawezavyo. ***(19: 14)***<br>2. Mungu alishuka kutoka Mbinguni katika umbo la moto - watu wa Israeli wakatetemeka kwa hofu chini ya nguvu zake. ***(19: 16-18)***<br>3. Mungu aliwaambia watu kwamba hawapaswi kuwa na mungu mwingine ila Yeye. ***(20: 3)*** Pia aliwaambia wasiabudu miungu mingine au sanamu, ambazo zingechukua nafasi Yake. Yeye ni Mungu mwenye wivu kwa ajili ya upendo wetu, na anaahidi upendo usiokoma kwa wale wampendao na kuzishika amri zake. ***(20: 5-6)***<br>4. Mungu anaposema ana wivu, wivu wake sio kama wa mwanadamu ambao ni dhambi. Wivu wa Mungu siku zote unaonyesha upendo wa kweli na kujali.<br>5. Pia hawakutakiwa kulitaja bure jina la Bwana. Namna tunavyolitaja jina Lake inatuonyesha jinsi tunavyohisi juu Yake. Tunapaswa kulitaja jina lake takatifu katika kusifu na kuabudu, sio kwa kusema vibaya au kuapa. ***(20: 7)***<br>6. Yesu alipokuwa duniani wakuu wa Sheria walijaribu kumtega. Waambie wanafunzi wasome ***Mathayo 22: 34-40***. Amri kuu ni ipi kulingana na maneno ya Yesu?<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Mungu mmoja. |
| **REJELEA SOMO** | Tafakari pamoja na wanafunzi jinsi Mlima Sinai ulivyo mahali patakatifu. Hapa alizungumza na Musa kwenye kijiti kinachowaka ***(Kutoka 3: 1-12)***. Mungu pia alizungumza na Eliya kwa sauti ndogo ya utulivu wakati alipokuwa amekimbia, akihofia maisha yake. ***(1 Wafalme 19: 1-13)*** | Jifunze Mstari Muhimu na jadili pamoja na kikundi jinsi huu mstari unavyotoa muhtasari wa funzo la leo. Uliza maswali ambayo yatawasaidia kumaliza funzo la kwanza. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Mungu ni mtakatifu sana na mkamilifu, na sisi ni wenye dhambi na wachafu kiasi kwamba tunahitaji njia ya kutuwezesha kumjia.<br>2. Hii ndiyo sababu Mungu alimtuma Mwanawe Yesu duniani ili atufie; ili dhambi zetu zisamehewe. Tunapokuwa na imani katika Bwana Yesu, Mungu anatuona kuwa tu safi na watakatifu! | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Waulize wanafunzi watafakari kama kuna kitu chochote katika maisha yao ambacho kinachukua nafasi ya Mungu au ni cha muhimu zaidi kwao kuliko Mungu? Labda wanapaswa kutafakari tena umuhimu wake.<br>2. Hoji iwapo wakati mwingine wanataja bure jina la Mungu na kulitaja kama neno la kiapo? Hili litamfanya Mungu ahuzunike sana. Wape changamoto wanafunzi kufikiria kwa umakini kuhusu jinsi wanavyolitaja jina Lake. |

| | **B11 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Pili – Musa**<br>**Mada – Kumjua Mungu** | **B11 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Pili – Sheria**<br>**Mada – “Njia ya Mungu”** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 20: 1-12***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 22: 37***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu ni Mungu mmoja wa kweli.<br>2. Jina la Mungu ni la pekee na linapaswa kuheshimiwa.<br>3. Jumapili inapaswa kudumishwa kama siku maalum ya kupumzika.<br>4. Ni muhimu kuwaheshimu mama na baba zetu. | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 20: 8-11, Luka 13: 10-17***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Kutoka 20: 8***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu anataka tuitunze Sabato kama siku takatifu.<br>2. Kufuata sheria hakupaswi kutuzuia kupenda watu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Fikiria kuhusu hali za kila siku ambapo kanuni ni jambo jema. Mfano. katika kucheza michezo, wazazi kuzuia watoto kugusa kitu cha moto, ishara za taa za barabarani, nyakati za kulala, kwenda shule, n.k Jadili na wanafunzi jinsi Mungu alivyowapa watu wa Israeli kanuni za kuwafanya wawe taifa lake takatifu - Amri Kumi. Walihitaji miongozo ya Mungu kuishi jinsi Mungu alivyotaka waishi. | Fikiria kuhusu hali za kila siku ambapo kanuni ni jambo jema Mfano, katika michezo, wazazi kuzuia watoto kugusa kitu cha moto, ishara za taa za barabarani, nyakati za kulala, kwenda shule, n.k Jadili na wanafunzi jinsi Mungu alivyowapa watu wa Israeli Amri Kumi za kuwafanya wawe taifa lake takatifu na kuwaonesha njia bora ya kuishi chini ya ulinzi Wake. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Amri ya Kwanza ***(mstari wa 1-3)*** ambayo Mungu aliwapa ilikuwa wasiwe na miungu mingine au sanamu zaidi ya Yeye. Sanamu ni kitu chochote ambacho kinachukua nafasi ya Mungu katika maisha yetu. Hii ilikuwa muhimu sana kwa Mungu; ndiyo sababu ni Amri ya Kwanza. Yesu mwenyewe alithibitisha hili katika ***Mathayo 4: 10.***<br>2. Amri ya Pili ***(mstari wa 4)*** ilikuwa kutotengeneza sanamu nyingine yoyote. Hii inaweza kuonekana kuwa ni rahisi, lakini watu wa Israeli ndio wamefika tu kutoka Misri, mahali ambapo kulikuwa na sanamu nyingi na miungu mingi. Yesu anasisitiza Amri hii katika ***Luka 16: 13.***<br>3. Amri ya Tatu ***(mstari wa 7)*** ilikuwa kutotaja bure jina la Bwana Mungu wetu. Jina la Mungu ni la pekee, hivyo halipaswi kutumiwa vibaya. Namna tunavyotumia jina lake inatuonyesha jinsi tunavyohisi juu Yake. Tunapaswa kutaja jina lake katika kusifu na kuabudu, sio kwa kusema vibaya au kuapa.<br>4. Amri ya Nne ***(mstari wa 8-11)*** ilikuwa kuitunza Sabato kama siku takatifu, tofauti na siku zingine sita za juma. Mungu aliumba mbingu na nchi kwa siku sita kisha akapumzika siku ya Sabato hivyo tunapaswa kufuata mfano wake. Mungu anataka tuwe na siku ya kupumzika na kumwabudu Yeye na uumbaji Wake.<br>5. Amri ya Tano ***(mstari wa 12)*** ilikuwa kuwaheshimu baba na mama zao. *Jadili maana ya heshima na jinsi tunavyoweza kuwaheshimu wazazi wetu.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kumjua Mungu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Moja ya Amri Kumi kwa Waisraeli ilikuwa kuishika siku ya Sabato na kuitunza kuwa takatifu, iliyowekwa wakfu kwa Mungu. ***(Kutoka 20: 8-11)***<br>2. Mungu mwenyewe aliumba mbingu na nchi kwa siku sita na kupumzika siku ya saba. Anatuhimiza tufanye vivyo hivyo na kuwa na siku moja kwa wiki tofauti na zingine, kuitumia kwa kupumzika na kumwabudu Yeye na uumbaji Wake. ***(Mwanzo 2: 2)***<br>3. Mungu alikuwa ameshaanza kuandaa utaratibu huu kwa Waisraeli kupitia maelekezo yao ya kukusanya mana. ***(Kutoka 16: 22-26)***<br>4. Yesu alipokuwa duniani, watu hawakufurahishwa na "utii" Wake wa Amri hii. Walimshtaki kwa kuvunja amri hii wakati alipoponya watu siku ya Sabato. Hii ilitokea mara nyingi. Mojawapo inapatikana katika ***Luka 13: 10-17.***<br>5. Yesu aliwaonyesha unafiki wao kwa vile wao wenyewe walihudumia wanyama wao siku ya Jumapili, lakini Je, Yesu hangeweza kumhudumia mwanadamu? Walikuwa wamefungwa sana na Sheria na kufuata Sheria kwa ukali kiasi kwamba walikuwa wamesahau mapenzi ya Mungu ni nini kwa ajili ya maisha yao.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Njia ya Mungu. |
| **REJELEA SOMO** | Soma ***Mathayo 22: 37-40*** na mjadili jinsi mistari hii inavyoweza kutoa muhtasari wa Amri Kumi. Uliza maswali kusaidia wanafunzi wakamilishe Somo la Pili. | Anzisha mjadala wa kikundi kuhusu kuitakasa Sabato na kuitofautisha na siku zingine ukiwa na makundi mawili; "Wanaokubali" na "Wanaopinga". |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Tunaweka miungu mingine au sanamu katika nafasi ya Mungu? Tunahitaji kuhakikisha kuwa vitu vingine k.v. michezo, Runinga, kazi, nk havichukui nafasi ya Mungu.<br>2. Je, tunaapa au kutumia jina la Mungu katika namna isiyofaa? Tunahitaji kuwa waangalifu kwa kulichukulia jina la Mungu kuwa ni la kipekee na takatifu.<br>3. Je! Tunaitunza Jumapili yetu kama siku maalum tofauti na zile zingine?<br>4. Je! Tunawaheshimu baba na mama zetu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Hakuna hata mmoja wetu anayeweza kushika Amri zote; sisi ni wenye dhambi na hatuwezi kufikia viwango vya Mungu peke yetu. ***(Warumi 3: 23)***<br>2. Hatuwezi kumpendeza Mungu kwa kujaribu tu kushika Amri hizi.<br>3. Yesu Kristo alikuja ili tuweze kupatana na Mungu, na akabeba adhabu ya dhambi zetu. Tunapompokea maishani mwetu, anatupatia Roho Mtakatifu ili atusaidie kuishi maisha yetu kama tunavyopaswa. |

| | B11 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Musa<br>Mada – Kumtii Mungu | B11 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Sheria<br>Mada – “Mungu kwanza” |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 20: 13-21; Mathayo 19: 16-30***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 19: 21***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alitoa Amri hizi ili tuzitii.<br>2. Kwa kutii Amri hizi, haimaanishi kwamba tutapata uzima wa milele.<br>3. Wakati mwingine tunaweza kutanguliza vitu vingine katika maisha yetu badala ya Mungu. | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 20: 12-21, Marko 10: 17-31***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 6: 24***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Amri na sheria ni muhimu na tunapaswa kuzitii.<br>2. Amri na sheria peke yake hazitaleta uhusiano na Mungu au uzima wa milele.<br>3. Ni rahisi sana kuweka sanamu zingine katika nafasi ya Mungu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Fikiria jinsi tunavyojaribu kutii kanuni shuleni lakini wakati mwingine tunasahau na kuzivunja. Pengine utoe mifano. Eleza kuwa hii ni kwa sababu sisi ni wanadamu na wenye dhambi kwa hiyo hatuwezi kuwa wakamilifu kama Mungu. | Fikiria jinsi tunavyojaribu kutii kanuni shuleni lakini wakati mwingine tunasahau na kuzivunja. Toa mifano. Eleza kwamba hii ni kwa sababu sisi ni wanadamu na wenye dhambi kwa hiyo hatuwezi kuwa wakamilifu kama Mungu. Hatuwezi kugharamia safari yetu ya kwenda Mbinguni kwa mambo tunayoyafanya. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Amri ya Sita haikuhusu kuua. Angalia ***Mathayo 5: 21-22*** ili uone ufafanuzi mpya wa Yesu wa kuua. *Fikiria jinsi hii inavyoathiri namna tunavyowatendea watu leo.*<br>2. Amri ya Saba haikuhusu kuzini.<br>3. Amri ya Nane haikuhusu kuiba. Katika Agano Jipya, Yesu anafafanua hii tena na anasema kwamba ikiwa mtu anakuibia shati lako, mpe pia kanzu yako! ***(Mathayo 5:40)***<br>4. Amri ya Tisa haikuhusu kutoa ushahidi wa uongo dhidi ya jirani yako. Waeleze wanafunzi kwamba hii inamaanisha kusema uongo kuhusu kile alichofanya mtu mwingine au kuacha sehemu ya habari nzima. *Tafuta **Mathayo 12: 36** ili uone kile Yesu alichosema juu ya jambo hili.*<br>5. Amri ya Kumi haikuwa kutotamani au kutokuwa na wivu juu ya kile ambacho watu wengine wanacho. Kutamani kunaonyesha upungufu wa tumaini kwa Mungu ambaye ni mpaji wetu.<br>6. Soma ***Mathayo 19: 16-30*** pamoja na wanafunzi. Jadilini jinsi Yesu anavyoonesha kwamba kushika Amri hizi zote hakumaanishi kwamba unarithi uzima wa milele. Wokovu hautokani na matendo mema tu bali kuna haja ya kuwa na upendo kwa Mungu, na utayari wa kuacha yote kwa kumtumaini Bwana Yesu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kumtii Mungu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yesu alipokuja duniani, Yeye alikuwa utimilifu wa Sheria na alibadilisha baadhi ya Amri: ***(Mathayo 5: 17-18)***<br>2. Amri ya Tano - waheshimu Baba na Mama yako - ***Mathayo 10:37*** inatuonyesha maono mapya ya Yesu juu ya hili.<br>3. Amri ya Sita - usiue. Angalia ***Mathayo 5: 21-22*** ili uone ufafanuzi wa Yesu wa kuua. *Fikiria jinsi hii inavyoathiri namna tunavyowatendea watu leo.*<br>4. Amri ya Saba - usizini. ***Mathayo 5: 27-28*** inatuonesha maelezo ya Yesu.<br>5. Amri ya Nane - usiibe. Yesu anafafanua hii pia. ***(Mathayo 5:40)***<br>6. Amri ya Tisa - usishuhudie jirani yako uongo. Waeleze wanafunzi kwamba hii inamaanisha kusema uongo juu ya kile ambacho mtu mwingine alifanya au kuacha sehemu ya habari nzima. Angalia ***Mathayo 12: 36*** ili uone kile Yesu alichokuwa anasema juu ya jambo hili.<br>7. Soma ***Marko 10: 17-31***. Jadilini jinsi Yesu anavyoonyesha kwamba wokovu hautokani na matendo mema lakini kuna haja ya kuwa na upendo kwa Mungu, utayari wa kuacha mali za kidunia na kuwa na imani kamili kwa Yesu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Mungu kwanza. |
| **REJELEA SOMO** | Katika vikundi vidogo, fikiria vitu ambavyo vinaweza kuwa katika maisha yetu ambavyo vinaweza kuwa muhimu zaidi kuliko Mungu, ambavyo vinatuzuia kumtanguliza Mungu. Jadili njia zinazofaa za jinsi tunavyoweza kuondoa vitu hivi, (sio lazima kuvitupa) ili kumtanguliza Mungu katika maisha yetu. (Angalia ***Mathayo 6: 33***) | Yesu alipokuja duniani, alikuwa mwana mapinduzi. Alifundisha kwamba matendo mema na kutii Amri vilikuwa havitoshi. Yesu alijitoa mwenyewe kama dhabihu ili dhambi zetu zisamehewe. Tunachopaswa kufanya ni kumtumaini na kumwamini kwamba alikufa kwa ajili yetu. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Tunadhani kwamba kama sisi ni wema na tunatii wazazi wetu, waalimu, n.k. kwamba Mungu atapendezwa na kwamba tutapata uzima wa milele? Angalia ***Waefeso 2: 8-9***<br>2. Je! Tutafanya makosa yaleyale ya yule kijana tajiri na kwenda zetu tukiwa na huzuni kwa sababu hatutaki kutoa vitu kwa ajili ya Mungu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Tunafanana na yule kijana tajiri tukidhani kuwa tu wema na tunashika sheria zote? Kushika sheria ni vyema lakini hakutatupa uzima wa milele au uhusiano na Mungu.<br>2. Tunapokea uzima wa milele kwa kumwamini Yesu, sio kwa kile tunachofanya. Bwana Yesu ndiye njia pekee ya sisi kumfikia Mungu. ***(Yohana 14: 6)*** (Tazama pia ***Waefeso 2: 8***) |

| | **B11 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Nne – Musa**<br>**Mada – Kumuasi Mungu** | **B11 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Nne – Sheria**<br>**Mada – “Neno la Mungu”** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Kutoka 32: 1-26***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Kutoka 32: 26***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Waisraeli walirudi nyuma wakaacha kumtii Mungu.<br>2. Mungu aliwaonyesha rehema wale waliomfuata na kuwaadhibu wale ambao hawakumfuata. | **Neno la Biblia:** ***Marko 7: 1-23***<br><br>**Mistari Muhimu:** ***1 Timotheo 1: 15, Warumi 5: 8***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mafarisayo walikuwa wanafiki.<br>2. Mapokeo hayapaswi kuwa muhimu zaidi kuliko Neno la Mungu.<br>3. Yesu aliwapa changamoto wafuasi wake kuhusu usafi wa mioyo yao. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waambie wanafunzi wafikirie juu ya wakati ambapo waliambiwa wasifanye jambo fulani…. Lakini hatahivyo wakaishia kulifanya! Matokeo yalikuwa nini? Eleza kwamba hiki ndicho kilichotokea hapa na kwamba Waisraeli walikuwa wamemsahau Mungu na kurudi kwenye kuabudu miungu ya uwongo. | Fikiria mapokeo ambayo tunayo, pengine katika familia zetu au kanisani. Baadhi ya haya mapokeo yanaweza kuwa mazuri na mengine yanaweza kuwa mabaya. Mapokeo mazuri yanaonesha nuru ya Neno la Mungu na kutupa msukumo wa kumtumikia na kumtii Mungu. Lakini hayapaswi kuwa muhimu zaidi kuliko Neno la Mungu. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Waisraeli walikosa subira ya kumngojea Musa ashuke kutoka Mlima Sinai. Kwa hiyo, walitengeneza miungu ya uwongo ili kuiabudu. ***(32: 1-4)*** Walitaka kufanya sanamu yao wenyewe ambayo wangeweza kuitawala wao wenyewe. Walikuwa tayari wamesahau Amri mbili za kwanza. ***(Kutoka 20: 1-5)***<br>2. Mungu alikuwa tayari kuharibu taifa lote kwa sababu ya kutotii na dhambi ***(32: 10)*** lakini Musa alimsihi Mungu asifanye hivi. Mungu anaonesha upendo na rehema zake hapa kwa kutowaangamiza wote. *Eleza maana ya rehema (kuepushwa na adhabu ambayo mtu anastahili)*.<br>3. Mungu aliwaonyesha rehema wale ambao walikuwa tayari kumfuata Bwana ***(32: 26)*** lakini kwa wale wengine, waliuawa kwa kutotii kwao.<br>4. Musa alikatishwa tamaa na Haruni kwa kupotosha watu wa Israeli. Alipaswa kujua kwamba kile watu wa Israeli walichokuwa wakifanya kilikuwa kibaya lakini badala yake alisikiliza manung’uniko yao na kuwasaidia kumtengeneza ndama huyu wa dhahabu wa kuabudiwa. ***(32: 22-24)*** *Je! Nyakati zingine tunafanya mambo ambayo tunajua si sawa, kwa sababu tu kila mtu anafanya hivyo?*<br><br>***Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.***<br>***Kamilisha Somo la Nne.***<br>***Onesha:*** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kumuasi Mungu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Wakati Yesu alipokuwa duniani, Sheria ambazo Musa na watu wa Israeli walikuwa wamepewa bado zilikuwa zikitumika. Hata hivyo, sheria na kanuni nyingi za ziada ziliongezwa kwa kufuata mapokeo kuhusu jinsi ya kuishi ambazo hazikutoka kwa Mungu.<br>2. Mafarisayo walikuwa watu wanaohukumu sana kwa hivyo walikuwa wamekuja kumchunguza Yesu. Waliwakosoa wanafunzi wa Yesu kwa kile walichofanya, wakidai kwamba walikuwa wakivunja sheria za Mungu. ***(Marko 7: 5)***<br>3. Mafarisayo walikuwa watu wanafiki. Matendo yao yalikuwa ya nje, ili watu wote wayaone na hayakutoka katika mioyo yao, na mioyo yao ilikuwa mbali na Mungu. Waliabudu kwa nia mbaya; kwa sababu walitaka kuonekana watakatifu na kuheshimika zaidi. ***(Marko 7: 6-8)***<br>4. Yesu aliwashutumu Mafarisayo kwa kutotii Sheria za Mungu, kwa sababu ya sheria zao wenyewe ambazo walikuwa wamezitunga Mfano, kutowajali tena mama na baba zao. Aliwakemea kwa kushika sheria na mapokeo ili kuonekana watakatifu badala ya kumheshimu Mungu. ***(Marko 7: 9-13)***<br>5. Yesu aliwafundisha wanafunzi umuhimu wa moyo safi na jinsi maisha yetu yanavyoweza kuwa na tabia ovu, zenye dhambi kama hatutafuti kuwa na moyo safi. ***(Marko 7: 17-23)***<br><br>**Elezea Mistari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Neno la Mungu. |
| **REJELEA SOMO** | Wape jaribio wanafunzi kuhusu habari ya leo kama njia ya kurejelea somo na kuwasaidia kulikamilisha. | Waambie wanafunzi waangalie ***Marko 7: 21-22*** na walinganishe na ***Wafilipi 4: 8***. Jadilini ni sifa zipi tunapaswa kuwa nazo katika maisha yetu na tunawezaje kuwa nazo? |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kama vile Mungu alivyowaonesha Waisraeli rehema Zake licha ya dhambi zao, sisi pia anaweza kutuonesha rehema Zake kama tunamuomba msamaha kwa ajili ya makosa ambayo tumefanya.<br>2. Mungu ni Mungu mwenye upendo na hataki kutuadhibu kwa dhambi zetu. Ndio maana alimtuma Mwanawe atufie ili tusipate adhabu ambayo tunastahili, na kwa kumtumaini Bwana Yesu tunaweza kusamehewa. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Hatupaswi kuwa wepesi kuhukumu na kushutumu watu bila kuangalia hali ya mioyo yetu wenyewe na nia zetu wenyewe. ***(Mathayo 7: 1-2)***<br>2. Hatupaswi kufungwa na sheria na mapokeo yetu na kuona kama ndiyo njia pekee ya kuishi kama walivyofanya Mafarisayo. Hali hii inaweza kutuzuia kumheshimu na kumpenda Mungu. Tukiwa na shaka, tunapaswa kumwangalia Bwana Yesu kwa ajili ya mwongozo kuhusu tabia zetu wenyewe. |

| | **B12 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Kwanza – Furaha ya Krismasi!**<br>**Mada – Ahadi za Mungu** | **B12 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Kwanza – Furaha ya Krismasi!**<br>**Mada – Kuzaliwa kwa Mwana** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Isaya 9: 1-7; Mika 5: 2***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Isaya 9: 6***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kuzaliwa kwa Yesu kulitabiriwa miaka mingi sana kabla ya kuzaliwa kwake.<br>2. Watu wengi walikuwa wakingojea kwa hamu kuzaliwa kwa Yesu.<br>3. Yesu ndiye Masihi aliyesubiriwa kwa muda mrefu, Nuru ya ulimwengu. | **Neno la Biblia:** ***Luka 1: 26-38; Luka 2: 1-7***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 1: 35***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kuzaliwa kwa Yesu kulitimiza unabii ulioandikwa miaka mingi iliyopita.<br>2. Mariamu na Yusufu walikuwa tayari kutumiwa na Mungu kama sehemu ya mpango Wake kwa ulimwengu.<br>3. Kuzaliwa kwa Yesu hakukujulikana sana huko Bethlehemu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize wanafunzi kama wamewahi kumfahamu mtu yeyote ambaye alikuwa mjamzito. Waeleze namna miezi 9 inavyoonekana mingi kwa wazazi kumsubiri mtoto azaliwe. Manabii walikuwa wamewaambia watu wa Israeli juu ya kuja kwa Yesu lakini walipaswa kungojea miaka mingi kabla ya kuzaliwa kwake. | Jadili na wanafunzi jinsi tunavyoweza kupanga mipango k.v. likizo, sherehe za kuzaliwa, harusi, kutembelea marafiki. Fikiria jinsi tunavyoitikia wakati mipango hii inapokwenda vibaya au inaposhindwa kwenda kama tunavyodhani ilipaswa kuwa. Jadili jinsi Mariamu alivyokuwa na mpango wa kuolewa na Yusufu lakini Mungu alikuwa na mpango mkubwa zaidi kwa ajili yake na Yusufu. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Jadili na wanafunzi jinsi ambavyo hatujui matokeo ya mechi ya mpira wa miguu yatavyokuwa kabla ya mchezo kuanza, au tutakachokuwa tunafanya katika kipindi cha miaka 40. Hatuwezi kutabiri hayo. Hata hivyo Isaya na Mika walikuwa wametabiri kuja kwa Yesu duniani, miaka mingi kabla ya matukio hayo kutokea.<br>2. Nabii Isaya anazungumza juu ya jinsi watu walio katika giza watakavyoona nuru kuu ambayo itawaangazia hata wale walio katika giza kuu. ***(Isaya 9: 2)*** Waulize wanafunzi wasome Yohana 8:12 ili kuona nani ni nuru hii kuu.<br>3. Waambie wanafunzi wasome ***Mathayo 4: 14-16*** ili kuona jinsi nabii hizi katika Isaya zilivyotimia, miaka mingi baadaye.<br>4. Jadili na wanafunzi jinsi mpango mkuu wa Mungu wa wokovu kwa ulimwengu ulivyokuwa wa ajabu na jinsi Wayahudi walivyokuwa wamesubiri miaka mingi ili mpango huu utimizwe. Wengi wao walikufa kabla ya kumwona amezaliwa. Fikiria jinsi iilivyo ajabu kwamba tuna habari ya maisha yote ya Yesu katika Biblia ili tuweze kumjua yeye kwa ajili yetu kama Mwokozi wetu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Ahadi za Mungu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu alimtuma malaika Gabrieli kumwambia Mariamu kwamba atapata mtoto. Mariamu anaogopa kwani yeye ni bikira na haelewi jinsi jambo hili litakavyotokea. Lakini malaika alimtuliza na kumwambia amepata neema kwa Mungu. ***(Luka 1: 26-34)***<br>2. Huenda Mariamu hakuelewa vizuri kile kilichokuwa kinafanyika, lakini alijua anapaswa kumtegemea Mungu. ***(1: 38)*** Jadilini tunapokeaje habari ambazo zinaweza kubadilisha kabisa maisha yetu milele.<br>3. Wakati Mariamu akiwa na tumbo kubwa la ujauzito, Mariamu na Yusufu walilazimika kusafiri kwenda Bethlehemu kutoka Nazareti kwa ajili ya sensa. Sensa hii iliamriwa na Augusto. ***(Luka 2: 1-5)*** Jadili jinsi Augusto alivyokuwa anadhani ni mtawala lakini kwa uhalisia, Mungu ndiye alikuwa anatawala, na hili lilikuwa sehemu ya wakati Wake na mpango Wake kwamba Bwana Yesu azaliwe Bethlehemu.<br>4. Yesu alizaliwa Bethlehemu ili kutimiza unabii wa Mika. ***(Mika 5: 2)*** *Fikiria kwa nini ilikuwa muhimu sana kwa Yesu kutimiza hizi nabii.*<br>5. Yesu anapozaliwa, Mariamu anamfunika nguo na kumlaza horini. ***(2: 7)***<br>6. Jadili jinsi ambavyo inawezekana Wayahudi wamekuwa wakisubiri Mfalme wao waliyemngojea kwa muda mrefu aje katika mazingira ya kifalme, lakini Yesu alizaliwa pamoja na wanyama. Eleza jinsi ambavyo hatupaswi kumwekea Mungu mipaka na kutarajia mambo yatokee kwa namna fulani. Hii ilikuwa sehemu ya mpango wa Mungu kwa Yesu. Alikuwa akiwaongoza Mariamu na Yusufu na kuwapa kila kitu wanachohitaji. Soma ***2 Wakorintho 8: 9.***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kuzaliwa kwa Mwana. |
| **REJELEA SOMO** | Soma ***Isaya 9: 6 & 7*** pamoja na wanafunzi na jadilini majina yaliyoorodheshwa ambayo Isaya alitabiri kwamba yatamzungumzia Yesu. Jadili pamoja na wanafunzi jinsi ambavyo Bwana Yesu angeweza kuitwa kila moja ya majina hayo. | Waombe wanafunzi wajione kama wao ni Mariamu au Yusufu. Waulize waandike kwenye kitabu cha kumbukumbu wakiwa na mtazamo kama Mariamu au Yusufu, kulingana na matukio kutoka kwenye funzo hili. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Waambie wanafunzi wafikirie juu ya sifa za nuru na jinsi Yesu anavyoweza kuitwa nuru ya ulimwengu. ***(Isaya 9: 2)***<br>2. Wape changamoto wanafunzi kumwona Yesu kama nuru ya ulimwengu. Tunapoona taa za Krismasi, labda zitatukumbusha kwamba Yesu ndiye Nuru ya Kweli, aliyetumwa duniani kutuokoa kutoka gizani na katika adhabu ya dhambi zetu.<br>3. Wanafunzi wanaweza kutengeneza kalenda ya ujio yenye jina tofauti au jina la Yesu, kwa ajili ya kila siku hadi Krismasi. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Pima uone kama wanafunzi wako tayari kama Mariamu kukubali mipango ya Mungu kwa ajili ya maisha yao, hata kama hatuielewi.<br>2. Tunamchukuliaje huyu Yesu, ambaye watu walikuwa wamemngojea kwa muda mrefu? Je! Tunamuona tu kama mtoto katika hori wakati wa Krismasi? Au ndiye Mwokozi ambaye unataka kumuishia kila siku? |

| | B12 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Pili – Furaha ya Krismasi!<br>Mada – Kustaajabishwa kwa Mariamu! | B12 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Pili – Furaha ya Krismasi!<br>Mada – Kutangazwa kwa Mwokozi |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 1: 26-38***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 1: 32***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Nabii kuhusu Yesu zilitimia, kuonyesha kwamba hii ilikuwa sehemu muhimu ya mpango mkuu wa Mungu.<br>2. Kama walivyokuwa Mariamu na Yusufu, sisi pia tunaweza kuandaa mipango yetu wenyewe lakini mipango ya Mungu kwa ajili ya maisha yetu ndiyo itatawala siku zote. | **Neno la Biblia:** ***Luka 2: 8-20***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 2: 11***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Malaika Mbinguni walifurahia kuja kwa Masihi yaani Kristo.<br>2. Wachungaji walifurahi kukutana na huyu mtoto Yesu baada ya kile walichosikia kutoka kwa malaika.<br>3. Sisi pia tunapaswa kusisimka na kusherehekea kuzaliwa kwa Yesu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadili na wanafunzi jinsi tunavyoweza kupanga mipango k.v. likizo, sherehe za kuzaliwa, harusi, kutembelea marafiki. Fikiria jinsi tunavyoitikia wakati mipango hii inapokwenda vibaya au inapokwenda tofauti na jinsi tunavyodhani ilipaswa kwenda. Jadili jinsi Mariamu alivyokuwa na mpango wa kuolewa na Yusufu lakini Mungu alikuwa na mpango mkubwa zaidi kwa ajili yake na Yusufu. | Fikiria juu ya namna ambavyo kwa kawaida kuzaliwa kwa mtoto kunatangazwa, labda na wazazi wao, kwa kadi au kwa picha za mtoto. Ni furaha kubwa. Eleza jinsi ambavyo Yesu hakuwa mtoto wa kawaida kwa hiyo kuzaliwa Kwake hakukutangazwa kwa njia ya kawaida! Kumbuka kwamba alikuja kwa ajili ya watu wa kawaida, kwa hiyo wachungaji walikuwa wa kwanza kusikia juu ya kuzaliwa Kwake. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu alimtuma malaika Gabrieli kwa Mariamu kumwambia kwamba atapata mtoto, ingawa bado hajaolewa. ***(mstari wa 26-31)***<br>2. Mariamu anasumbuka na haelewi jinsi jambo hili litakavyotokea, lakini malaika anamhakikishia kwamba amepata neema kwa Mungu na kwamba hakuna lisilowezekana kwa Mungu. ***(mstari wa 34-37)*** *Jadili na wanafunzi kwamba hii ilimaanisha nini.*<br>3. Onyesha uthibitisho muhimu kwamba Mariamu alitoka Galilaya na Yusufu alikuwa wa ukoo wa Daudi. Jadili na wanafunzi kwanini hili ni jambo muhimu sana; manabii walisema kwamba huyu Masihi Ajaye atatoka Galilaya ***(Isaya 9: 1)*** na atakuwa uzao wa Daudi. ***(Isaya 9: 7)*** Uthibitisho huu ulikuwa sehemu ya picha kubwa inayotimiza nabii zote.<br>4. Inawezekana Mariamu hakuelewa vizuri kile kinachotokea, lakini alijua kumtumaini Mungu. ***(mstari wa 38)*** Jadili jinsi ambavyo tungepokea habari kama hizi ambazo zingebadilisha kabisa maisha yetu milele.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kustaajabishwa kwa Mariamu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Usiku ambao Yesu alizaliwa, wachungaji walikuwa mashambani wakichunga kondoo zao. Onyesha kuwa kwa kawaida kunakuwa na ukimya na pengine uchovu wakati wachungaji wanapochunga kondoo usiku. ***(mstari wa 8)***<br>2. Lakini usiku ule, kitu cha ajabu kiliwatokea! Malaika aliwatokea na wote wakaogopa! Waulize wanafunzi jinsi ambavyo wangejisikia. ***(mstari wa 9)***<br>3. Malaika alikuwa amekuja kuwaambia kwamba Yesu, Mwokozi, amezaliwa. ***(mstari wa 11)***<br>4. Kisha malaika wengi zaidi walitokea pamoja na malaika huyo na wakamwimbia Mungu sifa, wakisherehekea kuja kwa Bwana Yesu duniani. *Eleza jinsi mwonekano huu ulivyokuwa mzuri kwa wachungaji, wakiwa gizani na kondoo.* ***(mstari wa 13-14)***<br>5. Mara malaika walipoondoka, wachungaji waliharakisha kwenda kujionea wenyewe mtoto huyu. *Fikiria jinsi walivyojisikia wakati huu; labda walidhani walikuwa wanawaza tu, au kwamba malaika alikuwa amekosea.*<br>6. Walimkuta mtoto kama vile malaika alivyoelezea! ***(mstari wa 16)*** Walimsifu na kumtukuza Mungu na wakaanza kumwambia kila mtu kuhusu Mwokozi aliyezaliwa. ***(mstari wa 17 na 20)***<br>7. Fikiria jinsi wachungaji walivyofurahi kumwona mtoto huyu na jinsi walivyoanza kuwaambia watu habari Zake mara moja bila kuchelewa na walivyotaka kushirikisha Habari Njema kwa wengine.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kutangazwa kwa Mwokozi. |
| **REJELEA SOMO** | Orodhesha ahadi zote ambazo malaika Gabrieli anatoa katika Mstari muhimu. Tunajifunza nini kutoka kwenye mstari huu kuhusu Mfalme ajaye na kile alichokuja kufanya? Je! Tunaamini kweli kwamba ahadi hizi zinamhusu Yesu? | Andaa bango au onyesho la ukutani kuhusu jinsi unavyofikiria tangazo hili la kuzaliwa lilivyoonekana. Jumuisha kile ambacho malaika alisema (Mstari Muhimu) katika onyesho lako. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Tuko tayari kama Mariamu kukubali mipango ya Mungu kwa ajili ya maisha yetu, ingawa tunaweza kutoielewa?<br>2. Tungemchukuliaje Yesu, ambaye watu walikuwa wamemngojea kwa muda mrefu?<br>3. Je! Tuko tayari kumtumaini Bwana katika maisha yetu ya baadaye, hata kama mipango yetu inaweza kutofanikiwa kama tunavyotaka? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Tunafurahi kama wachungaji kuwaambia wengine juu ya habari ya Yesu? Je! Unafikiri kweli kwamba kuzaliwa kwake ni kwa ajabu kama wao walivyoona?<br>2. Je! Tunasherehekea Krismasi kwa sababu sahihi? Je ni kuhusu tu zawadi na karamu au tunasherehekea kuja kwa Yesu duniani kuwa Mwokozi wetu? |

| | **B12 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Tatu – Furaha ya Krismasi!**<br>**Mada – Kuzaliwa kwa Yesu** | **B12 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Tatu – Furaha ya Krismasi!**<br>**Mada – Kusujudiwa kwa Mwenyezi** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 2: 1-7***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***2 Wakorintho 8: 9***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kuzaliwa kwa Yesu hakukutambuliwa vizuri huko Bethlehemu.<br>2. Yesu, Mwana wa Mungu alikuwa mwanadamu halisi.<br>3. Kuzaliwa kwake kulitimiza nabii zilizoandikwa miaka mingi iliyopita. | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 2: 1-12***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 2: 11***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alipozaliwa, wengine walimpokea wakati wengine hawakumpokea.<br>2. Mungu alikuwa akimjali Yesu, Mariamu na Yusufu na kuwahifadhi salama. |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadili na wanafunzi jinsi ambavyo wangejisikia kama mfalme au malkia angekuja kutembelea mji wao; pengine watu wangefurahi sana na wangefanya sherehe kubwa sana! Lakini Yesu alipozaliwa, hakuna mtu aliyejua. Haikujulikana. Hata chumba kwa ajili yake katika nyumba ya wageni hakikuwepo na kitanda chake kilikuwa hori. | Waulize wanafunzi wafikirie juu ya kile tunachofanya wakati mtoto anapozaliwa. Fikiria jinsi tunavyowanunulia zawadi, kwenda kuwatembelea, kumpakata mtoto. Eleza kwamba ni wakati wa furaha ya sherehe! |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Ilikuwa lazima Mariamu na Yusufu wasafiri kwenda Bethlehemu kutoka Nazareti kwa ajili ya sensa; kuhesabiwa na kusajiliwa. Fikiria jinsi ambavyo safari hii ndefu ilimchosha mwanamke mjamzito, hasahasa katika siku hizo. ***(mstari wa 1-4)***<br>2. Sensa hii iliamriwa na Augusto. *Jadili jinsi ambavyo inawezekana Augusto alifikiri anatawala kwa mamlaka yake mwenyewe, wakati kiuhalisia, Mungu ndiye alikuwa na mamlaka na, hii ilikuwa sehemu ya wakati Wake na mpango Wake.*<br>3. Wakiwa huko Bethlehemu, Yesu alizaliwa, akiwa pamoja na wanyama katika zizi na kulazwa horini. ***(mstari wa 7)***<br>4. Yesu alizaliwa Bethlehemu ili kutimiza unabii kwamba Masihi atazaliwa Bethlehemu. ***(Mika 5: 2)***<br>*Fikiria kwa nini ilikuwa muhimu sana kwa Yesu kutimiza unabii huu.*<br>5. *Jadili jinsi ambavyo hili halikuwa tukio la kawaida kwa mfalme kuzaliwa, lakini kwamba hili lilikuwa sehemu ya mpango wa Mungu kwa Bwana Yesu. Alikuwa akiwaongoza Mariamu na Yusufu na kuwapa kila kitu walichohitaji.*<br>6. *Jadili jinsi ambavyo Wayahudi wamekuwa wakimngojea mfalme wao aliyesubiriwa kwa muda mrefu kuja katika mazingira ya kifalme, na bado Yesu akazaliwa pamoja na wanyama. Eleza jinsi ambavyo hatupaswi kumwekea Mungu mipaka na kutarajia mambo yatokee kwa njia fulani.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kuzaliwa kwa Yesu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mfalme Herode alikuwa ndiye mfalme wakati Yesu alipozaliwa.<br>2. Mamajusi walikuwa wamesafiri kutoka Mashariki na walikuwa wameiona nyota iliyowaambia kwamba mfalme mpya amezaliwa. Wakamwuliza Mfalme Herode ni nani mfalme huyu. ***(mstari wa 1-2)***<br>3. Mfalme Herode alifadhaika kwa habari hiyo, kwamba kuna mfalme mwingine ambaye angeweza kuchukua nafasi yake kwenye kiti cha enzi. Hii ni kwa sababu hakuwa mfalme halali wa Israeli kwa kuzaliwa, kama Bwana Yesu alivyokuwa. Kwa hiyo alikuwa na mashaka na "mfalme" huyu. ***(mstari wa 3)***<br>4. Akawaambia mamajusi waende wamtafute mfalme huyu ili naye aende kumwabudu pia. Lakini Herode alikuwa amepanga kumuua mtoto huyo. ***(mstari wa 7-8)***<br>5. Mamajusi walifuata nyota na wakampata mtoto nyumbani Kwake. Pengine alikuwa na umri wa mwaka mmoja au miwili walipofika. Walipomwona, walifurahi sana! Wakamsujudia na kumpa zawadi za dhahabu, uvumba na manemane. ***(mstari wa 10-11)***<br>6. Mungu alikuwa amewaambia mamajusi katika ndoto wasafiri kurudi nyumbani kwa njia tofauti ili kumwepuka Mfalme Herode kwa vile alitaka kumuua Yesu. Walimtii Mungu na wakabadilisha njia yao ili kumlinda Yesu. ***(mstari wa 12)***<br>7. *Tafuta tofauti ya majibu ya mamajusi na ya Herode wakati wa kuzaliwa kwa Yesu. Walimtambua Yesu kama Masihi, Mwokozi wa ulimwengu, wakati Herode alimwona Yesu kama tishio kwa kiti chake cha enzi.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kusujudiwa kwa Mwenyezi. |
| **REJELEA SOMO** | Katika vikundi vidogo, andikeni makala kwa ajili ya gazeti la wenyeji wa Bethlehemu kutangaza kuzaliwa kwa Yesu. | Wape jaribio wanafunzi kuhusu funzo la leo kama njia ya kutathmini somo na kuwasaidia kwa kutumia Funzo la 3. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Watu hawakumtambua Yesu wakati alipozaliwa kwa sababu hawakujua habari zake. Sasa tunajua habari zake, lakini je! Tunamtambua? Je! Tunamuona tu kama mtoto katika hori wakati wa Krismasi? Au ndiye Mwokozi ambaye tunapaswa kutamani kumuishia kila siku?<br>2. Yesu alifanyika mwanadamu ili aende msalabani kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Je! Tunaelewa kweli ukuu wa mpango wa Mungu wa wokovu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Tunafanana na wale wenye hekima katika habari hii? Je! Tunamtafuta Bwana Yesu ili tumwabudu na kumpa zawadi? Au tunamtarajia atupatie zawadi na kutusaidia wakati sisi hatumpi chochote?<br>2. Hata leo watu wenye 'hekima' kama walivyokuwa mamajusi bado wanamtafuta na kumwabudu Yesu, sio kwa kile wanachoweza kupata Kwake lakini kwa vile Yeye alivyo. |

| | B12 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Furaha ya Krismasi!<br>Mada – Ujumbe wa Malaika | B12 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Furaha ya Krismasi<br>Mada – Wokovu! |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 2: 8-20***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 2: 11***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Malaika Mbinguni walifurahia kuja kwa Bwana Yesu, Mwana wa Mungu.<br>2. Wachungaji walifurahi kukutana na mtoto Yesu baada ya kile walichosikia kutoka kwa malaika.<br>3. Sisi pia, tunapaswa kufurahi na kusherehekea kuzaliwa kwa Yesu. | **Neno la Biblia:** ***Luka 2: 25-40***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Isaya 7: 14***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Watu walifurahi sana kuwasili kwa mtoto Yesu.<br>2. Kulikuwa na mwitikio wa aina tofauti kuhusu Yesu. Watu waliendaa kumpokea Yesu ama kwa furaha au kumkataa kabisa.<br>3. Bwana Yesu ndiye wokovu wa Mungu, aliyetumwa kuwa nuru ulimwenguni. |
| TOA UTANGULIZI | Fikiria jinsi kuzaliwa kwa mtoto kwa kawaida kunatangazwa, labda na wazazi wao, kwa kadi au kwa picha za mtoto. Kuna furaha ya kipekee. Eleza jinsi ambavyo Yesu hakuwa mtoto wa kawaida kwa hiyo kuzaliwa Kwake hakukutangazwa kwa njia ya kawaida! | Mtoto anapozaliwa, kunakuwa na msisimko mkubwa kwani watu wamekuwa wakimngojea kwa miezi tisa. Eleza kwamba watu ambao tunakwenda kujifunza habari zao katika Funzo hili walikuwa wamesubiri maisha yao yote ili kukutana na mtoto huyu ambaye alikuwa ameahidiwa – lazima walifurahi sana kwamba hatimaye amezaliwa! |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Usiku ambao Yesu alizaliwa, wachungaji walikuwa mashambani wakichunga kondoo zao. Onyesha kuwa kwa kawaida katika kuchunga usiku kondoo wanakuwa kimya na pengine wachovu kabisa. ***(Mstari wa 8)***<br>2. Lakini usiku huu, malaika aliwatokea na wote waliogopa! Waulize wanafunzi jinsi ambavyo wangejisikia. ***(mstari wa 9)***<br>3. Malaika alikuwa amekuja kuwaambia juu ya kuzaliwa kwa Yesu, Mwokozi. ***(mstari wa 11)***<br>4. Kisha malaika wengine walionekana pamoja na malaika huyu wakiimba sifa kwa Mungu, wakisherehekea kuja kwa Yesu duniani. ***(mstari wa 13-14)*** *Eleza jinsi maono haya yalivyokuwa mazuri kwa wachungaji.*<br>5. Mara malaika walipoondoka, wachungaji waliharakisha kwenda kumuona wenyewe mtoto. Fikiria jinsi walivyokuwa wanajisikia wakati huu; labda walidhani walikuwa wanawaza tu, au kwamba malaika alikuwa amekosea. ***(mstari wa 15)***<br>6. Walimkuta mtoto kama vile malaika alivyoelezea! Walimsifu na kumtukuza Mungu na kuanza kumwambia kila mtu kuhusu Mwokozi huyu ambaye amezaliwa. ***(mstari wa 16-17)***<br>7. *Fikiria jinsi wachungaji walivyofurahi kumwona mtoto huyu wa kiume na jinsi walivyoanza mara moja kuwaambia watu habari Zake.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Ujumbe wa Malaika. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Simeoni alikuwa mtu aliyemtii na kumwamini Mungu kwa bidii. ***(mstari wa 25)***<br>2. Roho Mtakatifu alikuwa amemuahidi Simeoni kwamba atamwona Masihi aliyesubiriwa kwa muda mrefu kabla ya kufa kwake. ***(mstari wa 26)*** *Jadili jinsi Simeoni alivyohisi wakati wa uzee wake, akijiuliza kama jambo hili litatimia au la.*<br>3. Siku moja, Simeoni alikuwa Hekaluni wakati Mariamu na Yusufu walipofika pamoja na mtoto Yesu.<br>4. Simeoni alifurahi sana, akamsifu Mungu, na kumbariki mtoto. ***(mstari wa 27-28)***<br>5. Katika ***Luka 2: 31-35*** Simeoni alisema kwamba mtoto huyo atakuwa furaha kwa watu wengi lakini kwamba wengi watampinga. Jadilini Simeoni alimaanisha nini kwa kusema hivi.<br>6. Anna, nabii, pia alikuwepo Hekaluni wakati huo huo. Siku zote alikuwa Hekaluni, akiomba na kufunga. ***(mstari wa 36-37)***<br>7. Alipomwona mtoto Yesu, alimsifu Mungu na kuanza kumwambia kila mtu habari Zake. ***(mstari wa 38)***<br>8. Yesu alikwenda nyumbani na wazazi wake na kukua katika kimo na hekima. Mungu alifurahishwa naye. *Eleza jinsi ambavyo Yesu alikuwa tofauti na watoto wengine wa umri sawa na Yeye.*<br>9. *Fikiria jinsi Mariamu na Yusufu walivyojisikia kuhusu namna Simeoni na Ana walivyomtendea mtoto wao.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Ajabu ya Krismasi. |
| REJELEA SOMO | Tengeneza bango au onyesho la ukutani kuhusu jinsi unavyodhani tangazo hili la kuzaliwa lilifanana. Jumuisha na kile ambacho malaika alisema (angalia Mstari Muhimu) kwenye onyesho lako. | Lazima Mariamu & Yusufu walihisi kuzidiwa na msisimko huu wa furaha ya mtoto wao wa kiume.<br>Jifunze Mstari Muhimu na jadili pamoja na kikundi jinsi mstari huo unavyotoa muhtasari wa Funzo la leo. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Tunafurahi kama wachungaji kuwaambia wengine kuhusu habari ya Yesu? Je! Ni kweli unafikiri kwamba kuzaliwa kwake ni kwa ajabu kama wao walivyofanya?<br>2. Je! Tunasherehekea Krismasi kwa sababu sahihi? Je! Ni kwa zawadi na karamu tu au tunasherehekea kuja kwa Yesu duniani kuwa Mwokozi wetu? ***(Angalia 2 Wakorintho 9; 15)*** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Simeoni na Anna walikuwa wacha Mungu. Je! Tunatoa maisha yetu kwa Mungu? Je! Tunamwomba Mungu na kusoma Biblia zetu?<br>2. Mstari muhimu, unasema Yesu anapaswa kuitwa "Imanueli" ikimaanisha "Mungu pamoja nasi". Kama tungeamini hivi, tungeishije maisha yetu? |

## Maelekezo ya waalimu wanaposahihisha masomo

**Masomo ya Daraja la Tatu**

- Wanafunzi hawawezi kukamilisha masomo haya bila kurejelea Biblia na wanaweza kulazimika kurejelea kifungu kimoja au zaidi vya Maandiko ya Biblia.
- Maswali yapo katika namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na jedwali la maneno, maneno yaliyokosekana, n.k.
- Masomo yametegenezwa kujibiwa kwa toleo la Biblia ya Kiswahili, Union Version iliyochapishwa kama "BIBLIA Maandiko Matakatifu".
- Lengo letu ni kwamba wanafunzi wote, waweze kujibu maswali kwa kutumia Biblia yoyote waliyo nayo.
- Alama ishirini zimetengwa kwa kila wiki ambapo kiwango cha juu kwa mwezi ni 80, pale masomo yanapokuwa ni sahihi kabisa.
- Daraja la tatu – Kwa kawaida na kama inavyooneshwa, alama 1 kwa kila jibu linalohitajika.

**Mafunzo ya Daraja la Nne**

- Masomo haya ni ya ngazi ya juu ya yale masomo ya Daraja la Tatu.
- Maswali ni ya kiwango cha juu na majibu ya kina zaidi yanahitajika.
- Alama ishirini kwa wiki na alama 80 kwa mwezi, wakati masomo yakiwa ni sahihi kabisa na maswali yana majibu kamili.

**VIDOKEZO VYA KUSAHIHISHA**

Walimu wanatakiwa, kwanza:

- Kukagua vizuri kila somo na kusahihisha majibu yaliyo sahihi au yasiyo sahihi.
- Toa alama kama ilivyoelekezwa.
- Kila mara, tumia kalamu ya rangi tofauti kusahihisha na kuweka ALAMA YA VEMA (✔) kwenye kila jibu sahihi.
- Weka au andika jibu sahihi panapostahili, na rekebisha makosa yoyote ya maandishi (spelling errors), lakini HAKUNA alama zinazoondolewa kwa ajili ya kosa hili.
- Toa alama chache kwa kila jibu ambalo sio sahihi kabisa.
- Jumlisha alama za mwezi na uandike kwenye nafasi iliyotolewa kwenye ukurasa wa mwisho.

Ni muhimu kuwa mkarimu kama uwezavyo ili kuwatia moyo watoto/ wanafunzi wafanye masomo ya Biblia. Kila mwezi, ni muhimu kwa mwalimu kuandika maneno ya kutia moyo kwenye nafasi iliyowekwa kwa kila mtoto anayemfundisha. Unaweza kuandika kuhusu kupaka rangi vizuri, kufanya kazi safi, alama alizopata mtoto, uelewa wa masomo wa mtoto na kadhalika.

Tunajaribu kutoa mawazo tofauti kama iwezekanavyo. Maswali, maoni, maneno ya kutia moyo na kadhalika, yote yanaweza kutumiwa kuleta utofauti. Kama maoni au usemi mmoja unatumika kila mwezi, watoto watauona hauna maana tena.

**Daraja la Tatu**

**Maoni ya jumla**

"Kazi njema! Ni wazi kwamba umesoma maswali kwa umakini sana. Nilipenda sana jibu lako la swali la mwisho ambalo lilikuwa limeandikwa vizuri. "

"Habari Yusufu. Hongera kwa kufanya kazi kwa bidii sana! Ilikuwa vizuri kwamba uliweza kujibu takriban majibu yote. Nimekujazia yale ambayo hayajakamilika."

**Maoni ya kiroho**

"Musa alikuwa na wakati mgumu na wana wa Israeli, lakini Mungu hakumwacha kutatua matatizo yote peke yake."

"Yusufu hakusahau kuwa baba yake alikuwa amemfundisha kumpenda Mungu. Alikumbuka hili hata alipokuwa mbali na nyumbani."

"Bartimayo alikuwa ameazimia kufika kwa Bwana Yesu. Hakujutia uamuzi wake kwani sasa alikuwa na uwezo wa kuona na sasa alijua kuwa Bwana Yesu alikuwa mtu wa pekee sana."

**Daraja la Nne.**

**Maoni ya jumla**

"Seti nyingine nzuri sana ya masomo. Unaonekana kuwa na ufahamu mzuri wa habari hizi za Biblia na ninatumaini kuwa umezifurahia. Asante kwa kutumia muda wako kufanya masomo kwa umakini. Ungeliweza kufanya masomo haya kwa haraka haraka, kwahiyo ninathamini juhudi zako zote."

"Neema, umejitahidi sana. Nadhani kwa majibu uliyoyatoa, pengine haukuweza kuelewa habari vizuri. Labda ungejaribu kuisoma tena."

**Maoni ya kiroho**

"Mifano ya Biblia wakati mwingine huitwa habari za kidunia zenye maana ya kimbingu, au maana ya ndani zaidi. Je! Unaweza kufikiria kuna maana gani ya kina katika mfano kwenye Funzo la Tatu?"

"Stefano alikufa kifo cha kikatili na bado hakuogopa kufa, kwa vile alijua kuwa Mungu bado anatawala kila jambo na alijua atakuwa na Bwana Yesu Mbinguni."

## Kiambatisho A – Picha za Bure za Biblia Daraja la Tatu

| | Kichwa | Picha za Habari |
|---|---|---|
| **B7** | **Yusufu** | **Wapelelezi nchi ya Misri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-ruler/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-brothers-1/ |
| | | **Benyamini na habari mbaya!** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-brothers/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-brothers-return/ |
| | | **Msamaha na habari njema!** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-reunion/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-jacob/ |
| | | **Pamoja huko Misri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-reunion/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-jacob/ |
| **B8** | **Waandishi wa Vitabu vya Injili** | **Mathayo** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-jesus-matthew/ |
| | | **Marko** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-man-leprosy/ |
| | | **Luka** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-ascension/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/jesus-birth/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-twelve/ |
| | | **Yohana** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/shepherds-sheep/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/jesus-5000/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-lazarus2/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/jesus-blind-man-pharisees/ |
| **B9** | **Musa** | **Mtoto kwenye kisafina** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-reunion/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/baby-moses/ |
| | | **Kosa lake kubwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-prince/ |
| | | **Kijiti kinachowaka moto** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-prince/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-burning-bush/ |
| | | **Kuleta ujumbe wa Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-pharaoh/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-plagues-1/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-plagues-2/ |

## Kiambatisho B – Picha za Bure za Biblia Daraja la Tatu

| | Kichwa | Picha za Habari |
|---|---|---|
| **B10** | **Musa** | **Mwanakondoo wa Pasaka** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-plagues-2/ |
| | | **Bahari ya Shamu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-red-sea/ |
| | | **Safari ngumu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/maps-egypt/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-food-water/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-amalekites/ |
| | | **Nyoka wa shaba** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-serpent/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bj-maps-egypt-canaan/ |
| **B11** | **Musa** | **Kukutana na Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-sinai/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-001-word-flesh/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/the-tabernacle/ |
| | | **Kumjua Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-objects/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-red-sea/ |
| | | **Kumtii Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-objects/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-rich-man/ |
| | | **Kumuasi Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-golden-calf/ |
| **B12** | **Habari ya Krismasi** | **Ahadi za Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/prophecies-birth-jesus/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/maps-israel-nt/ |
| | | **Kustaajabishwa kwa Mariamu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/mary-angel/ |
| | | **Kuzaliwa kwa Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/jesus-birth/ |
| | | **Ujumbe wa Malaika** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/shepherds-angels/ |

## Kiambatisho A – Picha za Bure za Biblia Daraja la Nne

| | Kichwa | Picha za Habari |
|---|---|---|
| **B7** | **Yusufu** | **Majaribu ya ujana wake** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-slave/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-potiphar/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-baker-cupbearer/ |
| | | **Kuinuliwa kwake ikulu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/pharaoh-dreams/ |
| | | **Tabia yake ya kujali** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-brothers/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-brothers-return/ |
| | | **Msamaha wake kamili** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-brothers-return/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-jacob/ |
| **B8** | **Njia iliyo mbele** | **Wakristo kuwa pamoja** |
| | | https://freebibleimages.org/illustrations/pentecost/ |
| | | **Ubatizo wa Kikristo** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/john-baptist/ |
| | | **Meza ya Bwana** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/last-supper-jesus/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/last-supper/ |
| **B9** | **Musa** | **Mwana wa Mfalme** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ten-minute-ot-1/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/baby-moses/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-prince/ |
| | | **Mchungaji** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-burning-bush/ |
| | | **Kiongozi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-pharaoh/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-plagues-1/ |
| | | **Mkombozi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-plagues-2/ |

## Kiambatisho B – Picha za Bure za Biblia Daraja la Nne

| | Kichwa | Picha za Habari |
|---|---|---|
| **B10** | **Musa** | **Kupitia Bahari ya Shamu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-red-sea/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bj-maps-egypt-canaan/ |
| | | **Juu ya Mlima Sinai** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-sinai/ |
| | | **Kutoka kwenye moto** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-golden-calf/ |
| | | **Jangwani** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bj-maps-egypt-canaan/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-serpent/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/hm-nicodemus/ |
| **B11** | **Sheria** | **Mungu mmoja** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-001-word-flesh/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-golden-calf/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-lazarus3/ |
| | | **Njia ya Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/jesus-alive/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-crippled-woman/ |
| | | **Mungu kwanza** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/jesus-teaching/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-rich-man/ |
| | | **Neno la Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-objects/ |
| **B12** | **Habari ya Krismasi** | **Kuzaliwa kwa Mwana** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/mary-angel/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bj-jesus-journeys/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/maps-israel-nt/ |
| | | **Kutangazwa kwa Mwokozi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/shepherds-angels/ |
| | | **Kusujudiwa kwa Mwenyezi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/wise-men/ |
| | | **Ajabu ya Krismasi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/simeon-anna-temple/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/prophecies-birth-jesus/ |

**© Bible Educational Services 2020**

**www.besweb.com**

**Registered Charity UK CIO 1186004**

**Swahili - 09/2023**